**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

**MHESHIMIWA ISSA HAJI USSI GAVU**
**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA**

**2020/2021**

**MEI, 2020**

# YALIYOMO

YALIYOMO ..................................................................... ii

ORODHA YA VIAMBATISHO ..................................................................... iii

VIFUPISHO VYA MANENO ..................................................................... iv

1. UTANGULIZI ..................................................................... 1

2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2019/2020 ..................................................................... 4

2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ..................................................................... 5

2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2019/2020 .......... 5

3. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ..................................................................... 31

4. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 32

5. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 ..................................................................... 39

6. HITIMISHO ..................................................................... 40

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida 2019/2020 ........... 44

Kiambatisho Nam. 2: Wageni Waliofika Ikulu Kuonana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia Mwezi Julai 2019 hadi Mwezi Aprili, 2020 ........................................ 48

Kiambatisho Nam. 3: Orodha ya vipindi vilivyorushwa hewani na Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu – Zanzibar kupitia Kituo cha ZBC Radio (A) ................................................................ 54

Kiambatisho Nam. 4: Orodha ya Shehia zilizooneshwa Sinema ...................................................... 57

Kiambatisho Nam. 5: Majina ya nchi wanachama za Jumuiya ya IORA ........................................ 59

Kiambatisho Nam. 6: Idadi ya Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo ................................................ 60

Kiambatisho Nam. 7: Idadi ya Watumishi waliokwenda likizo ......................................................... 64

Kiambatisho Nam. 8: Idadi ya wafanyakazi waliofanyiwa Upekuzi na Taasisi walizotoka ........... 65

Kiambatisho Nam. 9: Orodha ya Taasisi Zilizofanyiwa Ukaguzi wa Kiusalama .............................. 68

Kiambatisho Nam. 10: Idadi Watumishi Waliopewa Mafunzo ya Udhibiti wa Siri na Utunzaji wa Nyaraka za Serikali .............................................................................................................. 69

Kiambatisho Nam. 11: Orodha ya Nyaraka za Sera na Sheria zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi ........................................................................................................................... 70

Kiambatisho Nam. 12: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti 2020/2021 ............................ 71

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AfCFTA | African Continental Free Trade Area (Vikwazo visivyokua vya Ushuru Barani Afrika) |
| AU | African Union (Umoja wa Afrika) |
| BLM | Baraza la Mapinduzi |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| COMESA | Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika) |
| COVID - 19 | Corona Virus Disease (Maradhi ya Homa Kali ya Mapafu yanayoambukizwa na Virusi vya CORONA) |
| Dk | Doctor |
| DKT | Doctor of Philosophy |
| DRC | Democratic Republic of Congo (Jamhuri ya Demokrasia ya Watu wa Congo) |
| EAC | East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki) |
| GSO | Government Security Office (Ofisi ya Usalama wa Serikali) |
| IORA | Indian Ocean Rim Association (Jumuiya ya Nchi zilizopakana na Bahari ya Hindi) |
| IPA | Institute of Public Administration (Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar) |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar |
| KBLM/KMK | Katibu Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi |
| KIST | Karume Institute of Science and Technology (Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume) |
| MKUZA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar |
| MOU | Memorundum Of Understanding (Mkataba wa Makubaliano) |
| NTBs | Non - Tarrif Barries (Vikwazo vya Biashara visivyo ya Ushuru) |
| ORMBLM | Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi |
| PBZ | People's Bank of Zanzibar (Benki ya Watu wa Zanzibar) |
| PSA | Production Sharing Agreement (Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia) |
| SADC | Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika) |
| SDGs | Sustainable Development Goals (Malengo ya Mendeleo Endelevu) |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | State University of Zanzibar (Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar) |

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojioa ya Habari na Mawasilino |
| TZS | Tanzania Shillings (Shilingi ya Tanzania) |
| UAE | United Arabian Emirates (Umoja wa Falme za Kiarabu) |
| UNDP | United Nations Development Programme (Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Miradi ya Maendeleo) |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organizations (Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni) |
| UNFPA | United Nations Population Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mfuko wa Fedha kwa Watu) |
| US $ | United States Dollar (Shilingi ya Marekani) |
| VIP | Very Important Person (Mtu Mashuhuri) |
| VVU/UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| MBBS | Bachelor of Medicine and Bachelor of Surgery (Shahada ya Udaktari na Upasuaji) |
| ZACADIA | Zanzibar Canada Diaspora Association (Jumuiya ya Wanadiaspora wa Zanzibar wanaoishi Canada) |
| ZAECA | Zanzibar Anti - Corruption and Economic Crimes Authority (Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar) |
| ZAFICO | Zanzibar Fishing Corporation (Kampuni ya Uvuvi Zanzibar) |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Coorporation (Shirika la Utangazaji Zanzibar) |
| ZPDC | Zanzibar Petroleum Development Company (Kampuni ya Mafuta Zanzibar) |
| ZPRA | Zanzibar Petroleum Regulatory Authority (Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Zanzibar) |

## 1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. **Mheshimiwa Spika,** tunawajibu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie uhai na aendelee kuzilinda afya zetu sisi na familia zetu. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe uwezo na nguvu za kuijadili, kuichangia na hatimae kuipitisha hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nampongeza Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri uliojaa hekima na busara. Chini ya uongozi wake tumeshuhudia maendeleo makubwa hapa Zanzibar katika sekta mbali mbali ikiwemo miundombinu ya barabara, nishati, maji, kilimo, elimu na afya. Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein amedhihirisha uwezo wake wa kuwa jemedari katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020.

4. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, amekuwa Kiongozi wa mfano kwa kuwa karibu zaidi na Viongozi, Watendaji na Wananchi. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara na amjaalie afya njema yeye na familia yake.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo amemsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku ya kuongoza na kusimamia shughuli za Serikali katika kipindi chote cha awamu ya saba.

6. **Mheshimiwa Spika,** pongezi maalum nazitoa kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

weledi wake wa kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namuombea kwa Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema yeye na familia yake, ili aendelee kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ufanisi mkubwa zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa namna unavyoliongoza na kulisimamia Baraza lako Tukufu. Katika kipindi chako cha kuliongoza Baraza hili umehakikisha kuwa Waheshimiwa Wajumbe wote wanapata fursa sawa katika kuchangia hoja zinazowasilishwa Barazani. Kadhalika, tumeshuhudia nidhamu ya hali ya juu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa upande mwengine, nampongeza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar, Wenyeviti wa Baraza hili kwa namna wanavyokusaidia katika kukiendesha chombo hiki.

8. **Mheshimiwa Spika,** pongezi maalumu nazipeleka kwa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Panya Ali Abdalla pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (Shihata) kwa kuiongoza Kamati hii kwa uaminifu, hekima na busara. Vile vile, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hio kwa ushirikiano, ushauri na nasaha.

9. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Bajeti pamoja na Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza) Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Hesabu za Serikali. Vile vile, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo kwa ushirikiano wao walioutoa kwa ORMBLM. Tunakiri kuwa Kamati hizi zimekuwa zikifanya kazi kwa umakini na uwazi katika kuishauri na kuisimamia Serikali. Kadhalika, pongezi zangu mahsusi nazitoa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote kwa namna walivyoshirikiana na nasi wakati wa kuchangia Miswada, Taarifa na Hotuba za Bajeti za ORMBLM.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa unyenyekevu natoa shukurani zisizo na kifani kwa Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na kunipa jukumu la kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi na wananchi wote wa Jimbo letu la Chwaka.

11. **Mheshimiwa Spika,** nikiwa Mwakilishi wa wananachi wa Jimbo la Chwaka, pamoja na Mbunge Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Mensuria nachukua fursa hii adhimu kuwasilisha salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Chwaka zinazoelezea kufarajika kwao na kunufaika sana na uongozi wake. Wanakiri kuwa amekuwa ni Kiongozi wa mfano na aliyeongoza Zanzibar kwa hekima, busara na uvumilivu mkubwa. Vile vile, amehakikisha kuwa Amani na Utulivu inaendelea kulindwa na kudumishwa. Wanamuombea kila la kheri katika kulitumikia Taifa letu.

12. **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 28 Machi, 2020 Nchi yetu imepata msiba mkubwa kufuatia kifo cha Brigedia Jenerali Mstaafu Marehemu Ramadhani Haji Faki aliekuwa Waziri Kiongozi wa mwanzo wa Zanzibar na mmoja miongoni mwa watu 14 walioasisi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya 12 Januari, 1964. Namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amin.

13. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyoelewa kwamba, Dunia imekumbwa na janga kubwa la maradhi ya COVID – 19 yanayosababishwa na Virusi vya CORONA. Ugonjwa huo umepelekea watu wengi kuugua na kusababisha athari katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa upande wa Zanzibar wagonjwa kadhaa wamethibitishwa kuugua maradhi hayo na wengine kupona. Natoa pole kwa wale wote waliopata maambukizi haya pamoja na familia zote zilizopoteza wapendwa wetu.

14. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi za kipekee kwa Madaktari na Wahudumu wa afya kwa kujitolea kwa dhati katika kutoa huduma ya afya na tiba kwa walioambukizwa na maradhi hayo. Nawaomba waendelee kufanya kazi kwa uzalendo katika kupambana na janga hili. Nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe tuendelee kuchukua tahadhari zote za kujikinga na maradhi hayo, ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi majimboni

mwetu. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe shufaa na atuondoshee maradhi haya thakili.

**15. Mheshimiwa Spika,** msimu wa mvua tayari umenza katika visiwa vyetu. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia mvua kubwa zikinyesha katika maeneo yetu ambazo husababisha athari mbali mbali kwa wananchi zikiwemo nyumba na mali. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wananchi wote kuchukua tahadhari zinazostahiki, ili kujiepusha na athari zinazoweza kujitokeza. Kwa upande mwengine, nawaomba wananchi wazitumie vizuri mvua hizi kwa kupanda miti na mazao mengine ya chakula.

**16. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu niwasilishe Utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai – Machi, 2019/2020.

## 2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2019/2020

**17. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imetekeleza Programu Kuu tano na Programu Ndogo 11 chini ya Mafungu mawili ambayo ni Fungu A01 na A02. Programu Kuu hizo ni:-

i. (a) Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais,

(b) Kuimarisha Mawasiliano Ikulu,

ii. Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi,

iii. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

iv. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu na

v. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

**18. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hizi, umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015 – 2020, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA), Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 (Vission 2020) pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

## 2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilitengewa jumla ya TZS. milioni 11,726.5 kwa mafungu yake mawili. Fungu A01 lilitengewa jumla ya TZS. milioni 9,594.4. Kati ya hizo TZS. milioni 2000.0 kwa ajili ya mradi wa maendeleo na TZS. Milioni 7,594.4 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS. milioni 2,132.1. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Fungu A01 liliingiziwa jumla ya TZS. Milioni 6,312.0. Kati ya hizo TZS. Milioni 5,357.0 sawa na asilimia 71.0 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. milioni 955.0 sawa na asilimia 48.1 kwa ajili ya mradi wa maendeleo. Aidha, fungu A02 liliingiziwa 1,429.9 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 67 **(Kiambatisho Nam. 1)** kinatoa ufafanuzi.

## 2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2019/2020

### Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu

**20. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii iliidhinishiwa TZS. milioni 4,174.3 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 iliingiziwa jumla ya TZS. milioni 2,936.9 sawa na asilimia 70 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

21. **Mheshimiwa Spika,** katika programu hii, kwa kipindi hiki cha uongozi wake Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameiongoza Zanzibar kwa kuzingatia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sheria za Nchi pamoja na Misingi ya Utawala Bora.

22. **Mheshimiwa Spika,** wakati akitekeleza majukumu yake, Mheshimiwa Rais ameongoza vyema vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake, vilivyopelekea kuandaliwa kwa Sera na Miswada mbali mbali iliyowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa Rais ameendelea kupokea taarifa za utekelezaji wa ripoti za kila robo mwaka za kila Wizara ambazo zimeeleza utekelezaji wa kazi pamoja na upatikanaji wa fedha na ametoa maelekezo ya utekelezaji bora wa kazi hizo.

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa nafasi yake akiwa ni Mwenyekiti wa Tume ya Mipango amesimamia mipango ya Nchi na kuhuisha uchumi na kuufanya uendelee kukua kwa kasi hadi kufikia asilimia 7.1. Kadhalika, akiwa Mwenyekiti wa Baraza la Biashara ameweza kuzikutanisha Sekta Binafsi na Sekta ya Umma kufanya kazi kwa pamoja na kupata mafanikio makubwa katika uimarishaji wa biashara ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika wadhifa wake wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), ameendelea kukiongoza Chuo hicho na kuwa miongoni mwa Vyuo vilivyopata mafanikio makubwa.

25. **Mheshimiwa Spika,** shughuli nyengine ambazo zimetekelezwa ni uratibu wa ziara rasmi ya Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, aliyoifanya katika Umoja wa Falme za Kiarabu tarehe 22 hadi tarehe 29 Septemba, 2019. Mheshimiwa Rais alifanya ziara hio kwa mualiko wa Sheikh Saud Bin Saqr Al Qasimi, Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Falme za Kiarabu na Mtawala wa Ras Al Khaimah. Kimsingi ziara hio ilikuwa na lengo la kukuza ushirikiano zaidi baina ya Zanzibar na Ras Al Khaimah na Umoja wa Falme za Kiarabu kwa ujumla. Lengo jengine ni kushuhudia utiaji saini wa Mkataba wa Fedha za Msaada wa Dola za Kimarekani Milioni kumi (US$ 10,000,000) za Mfuko wa

"Khalifa Fund", kwa ajili ya kuwasaidia Vijana na Wajasiriamali wa Zanzibar, pamoja na Msaada wa Dola za Kimarekani Milioni kumi (US$ 10,000,000) kutoka Mfuko wa "Abu Dhabi Fund" kwa ajili ya kuifanyia matengenezo na upanuzi Hospitali ya Wete, Pemba.

**26.** **Mheshimiwa Spika**, akiwa Ras Al Khaimah, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikutana na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake, Sheikh Saud Bin Saqr Al Qasimi, Mtawala wa Ras Al Khaimah na Viongozi wengine Waandamizi wa Serikali. Katika mazungumzo yao, Viongozi hao wawili walikubaliana kuhusu kuimarisha ushirikiano katika sekta mbali mbali za maendeleo ikiwemo utafiti wa uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na sekta ya elimu.

**27.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mkataba wa Mgawanyo wa Mafuta na Gesi Asilia baina ya Ras Al Khaimah na Zanzibar, Viongozi hao walikubaliana utekelezaji wa Mkataba huo ikiwemo utafiti wa Rasilimali hizo uendelezwe. Vile vile, walikubaliana washirikiane katika kuzipitia Ripoti za Kitaalamu na Takwimu za utafiti wa mafuta na Gesi Asilia. Kwa upande wa sekta ya elimu, Ras Al Khaimah itawapatia walimu wa Zanzibar fursa ya mafunzo ya kujiendeleza hapa Zanzibar na katika Vyuo mbali mbali vya Ras Al Khaimah, kupitia Programu maalum itakayodhaminiwa na Serikali ya Ras Al Khaimah. Programu hio ya kila mwaka itakayoratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa Sera ya Sheikh Saud Bin Saqr Al Qasimi, ina lengo la kuwajengea uwezo Walimu wa Zanzibar hasa wa masomo ya Sayansi, ili kuwawezesha wanafunzi wa Zanzibar kufaulu vizuri katika masomo hayo. Maofisa kutoka Taasisi hio ya Utafiti wa Sera ya Sheikh Saud Bin Saqr Al Qasimi, walifika Zanzibar mwezi wa Novemba 2019, na kukutana na Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na taasisi za elimu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kukubaliana juu ya vipaumbele katika mahitaji ya kuwajengea uwezo walimu.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** katika ziara hio, Mheshimiwa Rais na Ujumbe wake alipata fursa ya kufanya mazungumzo na Viongozi wengine Waandamizi wa Taasisi mbali mbali ikiwemo Kampuni ya Uchimbaji mafuta na Gesi asilia ya Ras Al Khaimah (RAKGAS) na Taasisi ya Sheikh Saud Bin Saqr Al Qasimi inayoshughulikia Utafiti wa Sera. Kadhalika, mazungumzo na Uongozi wa

RAKGAS yalimjumuisha Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia, Bwana Nishant Dighe pamoja na wataalamu wa Kampuni hio. Katika mazungumzo hayo, Ujumbe wa Zanzibar ulielezewa kwa kina kuhusu kazi kubwa iliyokwishafanyika kufuatia shughuli zilizopangwa katika njia elekezi (Roadmap) ya mradi huo tangu ulipotiwa saini Mkataba wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (PSA), tarehe 23 Oktoba, 2018.

29. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa shughuli hizo ni mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi (ZPRA) na Kampuni ya Mafuta ya Zanzibar (ZPDC). Uongozi wa RAKGAS ulidhihirisha dhamira ya Kampuni yao ya kuendelea kufuata masharti ya Mkataba huo na kushirikiana na taasisi hizo katika kazi za mradi huo. Mheshimiwa Rais, aliutaka Uongozi wa RAKGAS, uje Zanzibar, ili ukutane na Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuwaelezea maendeleo yaliyofikiwa katika sekta hio. Uongozi huo ulikuja Zanzibar tarehe 5 Oktoba, 2019. Wakati huo huo, alipokuwa Ras Al Khaimah, Mheshimiwa Rais alibadilishana uzoefu na Kampuni pamoja na Taasisi mbali mbali katika uongezaji wa eneo la ardhi kwa kutumia utaratibu wa kufukia bahari (Land Reclamation), mafuta na gesi, masuala ya biashara, uwekezaji, viwanda, utalii na uendelezaji wa makaazi.

30. **Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara yake katika Umoja wa Falme za Kiarabu, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 28 Septemba, 2019, alikutana na alifanya mazungumzo na Mtawala wa Abu Dhabi na Naibu Amiri Jeshi Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi vya Umoja wa Falme za Kiarabu, Sheikh Mohammed Bin Zayed Al Nahyan. Kwa pamoja, Viongozi hao walishuhudia utiwaji wa saini wa Mkataba wa Msaada wa Dola za Kimarekani Milioni kumi (US$ 10,000,000), kwa ajili ya kuifanyia matengenezo na upanuzi Hospitali ya Wete, Pemba ambapo wananchi watafaidika kwa kuimarika huduma za afya. Vile vile, Mheshimiwa Rais na Mtawala wa Abu Dhabi, walizungumzia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika ziara iliyofanyika Januari, 2018 pamoja na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano. Ukiwemo ushirikiano katika nishati mbadala ya kutumia jua (solar energy); Kuimarisha sekta ya

Utalii na Uwekezaji pamoja na kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji Maji. Hatua za kufuatilia ushirikiano huo zinaendelea.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza na kuendeleza ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Rais alikutana na viongozi na watendaji mbali mbali katika Ikulu ya Zanzibar. Miongoni mwa viongozi hao ni Bwana Tirso Dos Santos, Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) nchini Tanzania, katika mazungumzo yao walikubaliana kuendelea kuimarisha urithi wa Kimataifa, ambapo Mji Mkongwe wa Zanzibar ni moja ya urithi wa Dunia. Vile vile, Mheshimiwa Rais alikutana na Bibi Jacqueline Mahon, Mwakilishi Mkaazi wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) nchini Tanzania, katika mazungumzo yao walikubaliana kuwa na Ushirikiano wa karibu kati ya Zanzibar na UNFPA. Wakati alipokutana na Bwana Alvaro Rodriguez, Mwakilishi Mkaazi wa Mpango wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Miradi ya Maendeleo (UNDP) nchini Tanzania, Mheshimiwa Rais alisisitiza uendelezaji wa ushirikiano baina ya Zanzibar na Taasisi mbali mbali za Umoja wa Mataifa zilizopo Tanzania. Katika mazungumzo yake na Dk. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa wanachama kushirikiana, ili kuzipatia ufumbuzi changamoto mbali mbali zinazozikabili Nchi wanachama.

32. **Mheshimiwa Spika**, Vile vile, Mheshimiwa Rais alikutana na Mheshimiwa Azali Assoumani, Rais wa Comoro, ambapo walikubaliana kuendeleza udugu na uhusiano wa kihistoria baina ya Nchi mbili hizi. Kadhalika, alikutana na Mheshimiwa Marcelino Medina Gonzalez, Naibu Waziri wa Kwanza wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Cuba na walikubaliana kushirikiana katika sekta ya afya na sekta nyengine za kijamii. Alipokutana na Mheshimiwa Guo Yezhou, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China, viongozi hao waliwafikiana kuendeleza udugu na urafiki ulioasisiwa na viongozi Wakuu wa Nchi hizo tangu 1964. Kadhalika, Mheshimiwa Rais alikutana na Mheshimiwa Jaji Sylvain Ore, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambapo, Mheshimiwa Jaji Ore aliipongeza Zanzibar kwa hatua kubwa zilizochukuliwa katika uimarishaji wa Haki za Binaadamu. Vile vile,

Mheshimiwa Rais alikutana na Bwana Mustapha Berraf, Rais wa Umoja wa Kamati ya Olimpiki za Afrika walizungumza suala la kuimarisha uwezo wa Zanzibar katika michezo.

33. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, kwa tarehe tofauti, Mheshimiwa Rais alikutana na kufanya mazungumzo na Waheshimiwa Mabalozi mbali mbali wanaoziwakilisha nchi zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kimsingi, Mabalozi hao wamempongeza Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri ambapo Zanzibar imefanikiwa kupata maendeleo na kuendelea kuwa nchi ya amani na utulivu. Orodha ya wageni waliofika Ikulu kuonana na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nam. 2.**

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya ziara katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Katika ziara hizo, Mheshimiwa Rais alikutana na Wazee na Viongozi wa CCM pamoja na Viongozi wa Serikali. Mheshimiwa Rais aliwataka Wazee wa CCM kuendelea kutoa taaluma kwa wananchi ya kuunga mkono Serikali katika kusimamia amani na utulivu, kutii sheria na kufanikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Vile vile, alihimiza umuhimu wa kuzingatia misingi ya demokrasia na utawala bora.

35. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, katika ziara hizo, Mheshimiwa Rais aliwahakikishia wazee kwamba viongozi na watendaji wataendelea kuelimishwa, ili watekeleze majukumu yao ipasavyo. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliwakumbusha viongozi na watendaji, juu ya umuhimu wa kuwasikiliza wananchi na kushirikiana nao katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili pamoja na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015-2020.

36. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 02 Julai, 2019, Mheshimiwa Rais alishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma. Mheshimiwa Rais aliwaeleza washiriki kuwa Utumishi wa Umma ulio bora ni chachu katika kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi yetu katika uchumi na uimarishaji wa

ustawi wa jamii. Kadhalika, Utumishi wa Umma ni kigezo muhimu cha misingi ya utawala bora na uimarishaji wa demokrasia nchini. Kwa hivyo, aliwahimiza watumishi wawajibike, wawe wazalendo, watunze siri na wawe wabunifu, ili waongeze ufanisi katika Utumishi wa Umma na kuchochea kasi ya maendeleo nchini.

37. **Mheshimiwa Spika,** wakati wa Mkutano wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), tarehe 8 Agosti, 2019, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa mgeni rasmi katika ufungaji wa Maonesho ya Nne ya Wiki ya Viwanda ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) yaliyofanyika Dar- es- Salaam. Mheshimiwa Rais alieleza kuwa maonesho hayo yataongeza fursa ya ushirikiano kati ya wenye viwanda wa nchi za SADC na watoa huduma wa mataifa mengine. Vile Vile, washiriki walitakiwa wajiongezee taaluma, maarifa na ubunifu utakaopelekea kuikuza sekta ya viwanda na biashara. Kadhalika, alisisitiza juu ya umuhimu wa wananchi katika nchi wanachama kununua bidhaa zinazotengenezwa katika nchi za SADC pamoja na kupongeza uamuzi wa kuifanya lugha ya Kiswahili iwe miongoni mwa lugha kuu nne rasmi za Jumuiya ya SADC ikiwa inatumika kama lugha ya kazi.

38. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 9 Septemba, 2019, Mheshimiwa Rais, kwa mara nyengine aliendeleza utaratibu wake wa kuwaandalia hafla maalum ya kuwapongeza wanafunzi bora waliopata daraja la kwanza katika matokeo ya mtihani wa Kidato cha Nne Novemba, 2018 na Kidato cha Sita Mei, 2019. Katika matokeo hayo jumla ya wanafunzi 375 wa Kidato cha Nne na wanafunzi 187 wa Kidato cha Sita walifaulu daraja la kwanza. Katika hafla hio, Mheshimiwa Rais aliwapongeza na aliwapa nasaha wanafunzi hao kuongeza bidii katika masomo yao kwa ngazi inayofuata. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliahidi kuongeza udhamini wa Serikali kwa wanafunzi bora wa kidato cha sita kutoka 30 hadi 60. Ahadi hio, tayari imeshatekelezwa.

39. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 14 Septemba 2019, Mheshimiwa Rais akiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) alikuwa Mgeni Rasmi katika sherehe za kuadhimisha miaka 18 tangu SUZA ilipoanzishwa,

zilizofanyika katika Kampasi ya Chuo Kikuu hicho Tunguu. Katika sherehe hizo, SUZA ilisherehekea kupatiwa Cheti cha Ithibati (Accreditation) ya kufundisha masomo ya Shahada ya Kwanza ya Udaktari ya MBBS na Shahada ya Pili ya masomo ya Udaktari Bingwa ya "Master of Medicine" (M.Med). Vile vile, SUZA ilisherehekea kupata Cheti cha kutambulika kwa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kuwa ni Hospitali ya Kufundishia Madaktari. Kutambulika huko kulifanywa na Bodi ya Afya ya Afrika Mashariki ya Baraza la Madaktari (East Africa Community Medical Boards and Councils). Katika hafla hio, Mheshimiwa Rais alisema kuwa kuanzishwa kwa Chuo Kikuu hicho ni matokeo ya kutafsiri kwa vitendo dhamira ya kuongeza fursa za elimu hapa Zanzibar baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari, 1964 ya kutoa elimu bure kwa watoto na Vijana wote wa Zanzibar.

40. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 10 Oktoba, 2019, Mheshimiwa Rais aliyafungua Maonesho ya siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika shughuli hio, Mheshimiwa Rais, alisema kuwa lengo la kufanya maadhimisho ya siku ya chakula Duniani ni kuihamasisha Serikali na taasisi mbali mbali kupanga na kutekeleza sera na mikakati ya kuimarisha sekta ya kilimo na kuwapa wananchi taaluma, ili pawe na usalama wa chakula na lishe bora nchini. Kadhalika, Mheshimiwa Rais alisisitiza uimarishaji wa taasisi za utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi na mipango ya Serikali ya kukiunganisha Chuo cha Kilimo Kizimbani kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), ili kuongeza idadi ya wataalamu na maafisa ugani.

41. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 22 Oktoba, 2019, Mheshimiwa Rais alifungua Mkutano wa 17 wa Jumuiya ya Majaji na Mahakimu wa Nchi za Afrika Mashariki uliofanyika katika Hoteli ya Madinat Al Bahar. Aliushukuru uamuzi wa Jumuiya hio wa kufanya mkutano huo Zanzibar kwa mara ya pili, baada ya mwengine kufanyika mwaka 2013. Alipongeza utaratibu wa vikao vya Jumuiya hio kufanywa kwa mzunguko na kusema kuwa inasaidia kuimarisha uhusiano mwema wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kadhalika, alisema kuwa juhudi zetu za kuimarisha mtangamano wa kiuchumi wa nchi wanachama, lazima ziende sambamba na kuimarisha utendaji wa vyombo vya sheria hasa Mahkama.

42. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 29 Oktoba, 2019, Mheshimiwa Rais alizindua kadi mpya ya kielektroniki ya Mzanzibari Mkaazi katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, shughuli ambayo ilitanguliwa na ziara ya ukaguzi wa Ofisi inayoshughulikia utoaji wa huduma za kadi hizo iliyopo Mazizini. Katika hotuba yake, alisema kuwa utaratibu wa kutumia vitambulisho vya uraia na ukaazi una umuhimu wa kuzihifadhi kumbukumbu za matukio ya watu wote katika Daftari la usajili na utambuzi. Vile vile, utaratibu huo utaisaidia Serikali kuwatambua watu wanaostahili kupata haki zao za msingi, kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Aliwataka wananchi kufuata taratibu na kuzingatia sheria katika kufuatilia upatikanaji wa kadi hizo ambazo ubora wake umeimarishwa kwa kuzingatia teknolojia ya kisasa.

43. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 18 Novemba, 2019, Mheshimiwa Rais alikuwa Mgeni Rasmi katika hafla ya ufunguzi wa Maonesho ya Wajasiriamali Juakali/Nguvukazi kuadhimisha miaka 20 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hafla hio ilifanyika Fumba, Zanzibar ambapo katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alisisitiza hoja ya kudumisha umoja, amani na utulivu katika kuunga mkono utawala wa sheria katika nchi za Afrika Mashariki, ili eneo hili liimarike kiuchumi kwa kutumia ujuzi, maarifa na ubunifu.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha shughuli za uwekezaji na kushajiisha sekta binafsi, tarehe 27 Novemba, 2019 Mheshimiwa Rais alishiriki katika hafla ya uzinduzi wa boti ya Kilimanjaro VII inayomilikiwa na Kampuni ya Azam Marine, shughuli iliyofanyika katika Hoteli ya Verde, Mtoni Zanzibar. Mheshimiwa Rais, alieleza kuwa Serikali itaendelea na juhudi za kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji wazalendo wanaotaka kuwekeza katika miradi mbali mbali. Vile vile, alieleza jitihada za Serikali katika kuimarisha usafiri wa baharini na kukabiliana na changamoto zinazoihusu sekta hio.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika mwezi wa Disemba, 2019, Mheshimiwa Rais aliungana na Viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi katika sherehe za Uhuru na Jamhuri za iliyokuwa Tanganyika zilizofanyika katika uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. Akiwa katika hafla hio, alitoa salamu zake kwa Wananchi ambapo aliwataka Watanzania kuulinda Muungano wa Tanzania ambao ni imara na wenye faida nyingi kwa

wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Aliwahakikishia wananchi kuwa Muungano huo wa Serikali mbili utaendelea kudumu. Kadhalika, akiwa jijini Mwanza Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure na ufunguzi wa Kituo cha Afya - Igoma, katika Wilaya ya Nyamagana. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliifunguwa rasmi Nyumba ya makaazi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binaadamu yaliyofanyika tarehe 16 Disemba 2019 kwenye ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Mheshimiwa Rais akiwa mgeni rasmi, alisema kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi nyingi duniani zilizoamua kuzilinda haki za binaadamu jambo ambalo limebainishwa wazi katika sura ya Tatu ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na sehemu ya Tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliongeza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, imefanya jitihada kubwa za kuhakikisha misingi ya Utawala Bora ambayo ni ushirikishwaji wa umma, utawala wa sheria, haki na usawa kwa wananchi wote, uadilifu na uwazi inazingatiwa katika kuendesha shughuli za maendeleo, ili kukuza uchumi na kujenga jamii yenye imani, upendo na mshikamano.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine, tarehe 31 Disemba, 2019 Mheshimiwa Rais akiwa Mkuu wa Chuo alihudhuria sherehe za Mahafali ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), yaliyofanyika katika Ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein, kampasi ya Tunguu. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais akiwa ni Mkuu wa Chuo hicho alipongeza mafanikio ambayo Chuo hicho kimeyapata ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa watumishi wa chuo wa kada mbali mbali waliofikia 637, ongezeko la majengo ya Chuo, na programu za masomo zinazofikia 62 kutoka mbili za mwanzo. Vile vile, alisema siri kubwa ya mafanikio hayo ni kuwepo kwa moyo wa kujituma na uzalendo, uwajibikaji, ushirikiano na ubunifu wa mambo ambayo alihimiza yandelezwe, ili tuweze kuyafikia malengo na dira ya taasisi hio ya Umma ya elimu ya juu hapa Zanzibar.

48. **Mheshimiwa Spika,** katika risala ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2020, Mheshimiwa Rais pamoja na mambo mengine, aliwapongeza wananchi kwa kuendelea kushirikiana na Serikali zote mbili katika utekelezaji wa mipango mikuu ya maendeleo na kudumisha amani na utulivu. Katika risala hio, alieleza maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kwa asilimia 7.1 katika mwaka 2018 ikilingalishwa na asilimia 6.8 kwa mwaka 2016. Vile vile, alitaja mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita katika sekta nyengine ikiwemo kilimo, uvuvi, ufugaji, mafuta na gesi asilia, elimu, afya na uimarishaji wa miundo mbinu ya barabara pamoja na ujenzi wa miji. Mheshimiwa Rais, alitoa pole kwa wananchi waliopata maafa kutokana na upepo mkali uliombatana na mvua iliyotokea usiku tarehe 21 Disemba, 2019.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika kuadhimisha miaka 56 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, Mheshimiwa Rais alishiriki shughuli mbali mbali ikiwemo uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi wa miradi ya maendeleo na matukio yaliyopangwa katika kufanikisha sherehe hizo ambazo zilifikia kilele tarehe 12 Januari, 2020 ambapo Mheshimiwa Rais, alikuwa Mgeni Rasmi.

50. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 1 Januari 2020, Mheshimiwa Rais alishiriki katika matembezi na mazoezi ya Viungo yanayofanywa kila mwaka yaliyoanzia maeneo ya Ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil Kikwajuni na kumalizia katika viwanja vya Mao Dzedong. Katika shughuli hio, Mheshimiwa Rais alisema michezo ina uhusiano mkubwa na harakati za ukombozi wa Zanzibar. Tarehe 5 Januari, 2020, Mheshimiwa Rais aliifungua Skuli ya Sekondari ya Dk. Ali Mohamed Shein, Rahaleo, Unguja kwa niaba ya skuli nyengine 8 za ghorofa zilizojengwa katika maeneo ya Unguja na Pemba. Vile vile, tarehe 7 Januari 2020, aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Ziwakije na Wingwi, katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika hafla hizo, Mheshimiwa Rais alisisitiza juu ya Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kutoa elimu bure ikiwa ni miongoni mwa matunda ya Mapinduzi.

51. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 6 Januari, 2020, Mheshimiwa Rais aliufungua Mradi wa tangi la Maji Safi na Salama liliopo Mnara wa Mbao na Saateni

katika Mkoa wa Mjini Magharibi, shughuli iliyofanyika Saateni katika maeneo ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Katika hotuba yake, alielezea furaha yake kwa kukamilika kwa mradi huo ambao ni mkombozi mkubwa wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Shehia 11 za Jiji la Zanzibar. kwa upande mwengine, tarehe 8 Januari, 2020 katika viwanja vya Ikulu Zanzibar, Mheshimiwa Rais kwa kutumia uwezo aliopewa katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Mambo ya Rais namba 5 ya mwaka 1993, alitunuku Nishani 72 kwa wananchi wenye sifa. Jumla ya wananchi 37 walitunukiwa Nishani ya Mapinduzi, 10 Nishani ya Utumishi uliotukuka na 25 Nishani ya Ushujaa.

52. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 9 na 10 Januari, 2020, Mheshimiwa Rais alifungua daraja jipya la Dk. Ali Mohamed Shein la Kibonde Mzungu na barabara ya Bububu hadi Mkokotoni yenye urefu wa kilomita 31. Hatua hizo ni muhimu katika maendeleo ya sekta ya miundo mbinu ya barabara kwani imewaondoshea usumbufu wananchi. Kadhalika, shughuli nyengine alizofanya Mheshimiwa Rais katika maadhimisho ya miaka 56 ya Mapinduzi ni kuweka jiwe la msingi la Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Kilimo cha Mpunga wa Umwagiliaji Maji katika Wilaya ya Kaskazini "A", jiwe la msingi la Majengo ya Biashara (Shopping Malls) Michenzani na Mwembe Kisonge, jiwe la msingi la Mradi wa Ujenzi wa Bandari na Soko la Samaki Malindi pamoja na jiwe la msingi la Ujenzi wa Mji Mpya wa Kwahani.

53. **Mheshimiwa Spika,** shamra shamra za maadhimisho ya Sherehe miaka 56 ya Mapinduzi zilijumuisha maandamano na maonesho ya Amsha Amsha na Mapinduzi yaliyoandaliwa na Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Idara Maalumu za SMZ. Shughuli hio ilifanyika tarehe 11 Januari, 2020 na iliishia katika viwanja vya Mnazimmoja. Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake aliwahakikishia wananchi kwamba ulinzi na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upo imara, na Serikali zote mbili hazitovumilia kuona kuwa kuna watu wanaichezea amani ya nchi, kukejeli Mapinduzi na Muungano, ambayo ni nguzo muhimu za maendeleo ya nchi yetu.

54. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 12 Januari, 2020, Mheshimiwa Rais alikuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha Sherehe za Miaka 56 ya Mapinduzi Matukufu

ya Zanzibar, zilizofanyika katika uwanja wa Amaan. Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais alielezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 56 ya Mapinduzi ikiwemo ukuaji wa uchumi, kuimarika kwa huduma za elimu, afya, maji safi na salama, kilimo, ufugaji na uvuvi, michezo na utamaduni pamoja na sekta nyengine za maendeleo. Aliwahimiza wananchi waendelee kuitunza amani, umoja na mshikamano pamoja na kufanyakazi kwa bidii na uzalendo.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika maendeleo ya sekta ya sheria Zanzibar, tarehe 10 Februari, 2020 Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa jengo jipya la Mahkama Kuu ya Zanzibar huko Tunguu. Pamoja na mambo mengine, alielezea jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha utendaji mzuri wa Mahkama. Alieleza kuwa ana imani kubwa kuwa, wananchi wa Zanzibar wanaziamini Mahkama zao na hivyo wanaendelea kuzipa ushirikiano hasa katika kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji. Vile vile, tarehe 11 Februari, 2020 Mheshimiwa Rais alishiriki katika maadhimisho ya siku ya Sheria, katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni. Katika hafla hio, Mheshimiwa Rais alihimiza wananchi wazingatie sheria zinazoendana na taratibu za shughuli za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Kadhalika, alisisitiza haja ya wananchi kushiriki katika uchaguzi huo kwa amani katika hatua zake zote, jambo ambalo ni wajibu wa wananchi wote.

56. **Mheshimiwa Spika,** tarehe 7 Machi, Mheshimiwa Rais akiwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Zanzibar, aliongoza kikao cha Jukwaa la Kumi la Biashara Zanzibar, katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni. Aliwaambia wajumbe wa Jukwaa hilo kuwa upatikanaji wa ufumbuzi wa changamoto za uendeshaji wa biashara kwa haraka, utaondoa vikwazo vinavyokwamisha maendeleo ya biashara. Hali hio itachangia kuharakisha maendeleo ya ukuaji wa uchumi kwa kufikia kiwango cha uchumi kwa wakati kama inavyotarajiwa.

57. **Mheshimiwa Spika,** katika suala zima la kuendeleza sanaa na utamaduni, Mheshimiwa Rais tarehe 17 Machi, 2020, alifanya mkutano na Wasanii wa Zanzibar wa fani mbali mbali katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil. Mheshimiwa Rais aliwapongeza wasanii hao kwa kazi nzuri wanayoifanya na

kuwahakikishia kuwa Serikali inazithamini jitihada zao na itaendelea kuwapa ushirikiano. Vile vile, alieleza jitihada mbali mbali zinazofanywa na Serikali katika kuziimarisha sekta hizo ikiwemo ujenzi wa Studio mpya ya kurikodia filamu ya Rahaleo na kuhakikisha kuwa wasanii na wabunifu wa Zanzibar wananufaika na kazi zao kwa kupata mirabaha wanayostahiki.

**58. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha sekta ya afya, mnamo tarehe 25 Machi, 2020 Mheshimiwa Rais alifanya ziara maalum huko Binguni Wilaya ya Kati kulikagua jengo linalojengwa kuwa maabara maalum ya uchunguzi na utafiti wa virusi ambapo uchunguzi wa COVID - 19 utafanyika. Akiwa katika eneo hilo, Mheshimiwa Rais alieleza dhamira ya Serikali ya kujenga jengo hilo katika kipindi cha miezi mitatu. Vile vile, aliwaasa wananchi wachukue tahadhari ya ugonjwa wa COVID - 19 kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya na Serikali. Kadhalika, aliwaasa wananchi waache mzaha na ukaidi juu ya maradhi hayo kwani yana athari kubwa na tayari yamewaathiri watu wengi duniani.

**59. Mheshimiwa Spika,** tarehe 23 Aprili, 2020 sawa na mwezi 29 Shaabani 1441, Mheshimiwa Rais alitoa risala ya kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramdhani. Pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais aliwataka wananchi kuupokea mwezi huo kwa kufanya ibada kwa wingi, kuchukua tahadhari ya kupambana na ugonjwa wa COVID - 19 na aliwasisitiza wafanyabiashara wasiongeze bei ya bidhaa hasa katika kipindi hiki. Vile Vile, aliwatakia Waislamu na wananchi wote kila la kheri katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

**60. Mheshimiwa Spika,** wananchi wameendelea kupewa taarifa za shughuli za Mheshimiwa Rais kupitia vyombo mbali mbali vya habari nchini, mitandao ya kijamii, jarida la Ikulu na kalenda. Katika kipindi hicho, vipindi 20 vya radio na vipindi 28 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar **(Kiambatisho Nam. 3)**. Vipindi hivyo vilielezea mafanikio na hatua zilizofikiwa katika kuimarisha sekta ya Elimu, Miundombinu, Kilimo na Maji.

**61. Mheshimiwa Spika,** Kipindi kipya cha mijadala (Ikulu Talk Show) kwa kuwashirikisha wanafunzi wa Sekondari zimeandaliwa na kurushwa hewani

na Shirika la Utangazaji ZBC. Mijadala hio imezungumzia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Sekta ya Elimu, Afya, Miundombinu ya barabara na ardhi, maji na nishati.

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, taarifa juu ya utekelezaji wa Mipango ya Serikali zimetolewa kupitia maonesho ya Sinema ambapo jumla ya Shehia 29 zimefikiwa (12 Pemba na 17 Unguja). **Kiambatisho Nam. 4** kinatoa ufafanuzi zaidi. Vile vile, matangazo ya moja kwa moja yanaendelea kurushwa hewani katika ziara na mikutano yote ya Mheshimiwa Rais kupitia ukurasa wa "facebook" wa Ikulu habari Zanzibar, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Bahari FM.

63. **Mheshimiwa Spika,** Wananchi wetu wanaendelea kupata taarifa za matukio mbali mbali yanayofanyika nchini. Taarifa hizo hutolewa kupitia nakala za kalenda zinazochapishwa kila mwaka. Kwa kipindi hicho, nakala 7,000 za kalenda zimeandaliwa, kuchapishwa pamoja na kusambazwa katika Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi na Vituo vya Walimu Unguja na Pemba. Vile vile, matoleo ya jarida la Ikulu namba 43, 44, 45 na 46 ambayo ni sawa na nakala 12,000 zimechapishwa na kusambazwa. Aidha, wananchi wa kawaida nao wamepatiwa jarida hili kupitia Ofisi za Masheha na mikusanyiko ya watu mbali mbali.

64. **Mheshimiwa Spika,** kupitia utekelezaji wa programu hii, wananchi wamepata taarifa sahihi juu ya mipango ya Serikali na utekelezaji wa miradi mbali mbali inayotekelezwa. Kadhalika, wananchi wamepata fursa ya kutoa maoni yao juu ya namna bora ya kufikiwa na kuwasilisha taarifa kwao. Vile vile, wanafunzi wa Sekondari wamepata Jukwaa la kujadili kwa kina na kubadilishana mawazo juu ya maendeleo yaliyopatikana katika Awamu ya Saba.

**Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi**

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 648.3 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Programu hii iliingiziwa jumla ya TZS. milioni 465.8 sawa na asilimia 72 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

66. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umeipelekea Zanzibar kuimarisha ushirikiano pamoja na kushiriki mikutano ya Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda za EAC, SADC, IORA na AfCFTA. Ushirikiano huo umeimarika katika maeneo ya biashara, uwekezaji, utalii na uchumi wa bahari.

67. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kutekeleza diplomasia ya Kiuchumi Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kuendeleza jitihada za ndani na za Kimataifa za kujipatia na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kuleta amani ya kweli na utulivu nchini na duniani kote.

68. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshiriki mikutano mbali mbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Mkutano wa 30 wa Kisekta wa Baraza la Mawaziri wanaohusika na masuala ya Afrika Mashariki na Mipango uliofanyika tarehe 07 hadi 12 Oktoba, 2019 Jijini Arusha, Tanzania. Miongoni mwa masuala yaliojadiliwa katika mkutano huo ni tathmini ya utekelezaji wa maamuzi na maelekezo ya Mikutano ya Kilele ya Wakuu wa Nchi pamoja na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mshariki iliyopita. Kadhalika, mkutano huo ulijadili hatua za utekelezaji wa mipango na mikakati ya Jumuiya na hatua zilizofikiwa pamoja na kupendekeza mikakati ya kufanikisha hatua za baadae za utekelezaji.

69. **Mheshimiwa Spika,** maeneo ambayo yalionekana utekelezaji wake kuendelea kuwa na changamoto ni utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja katika kurekebisha sheria za Nchi Wanachama kuendana na sheria za Jumuiya, mapendekezo ya viwango vipya vya Umoja wa Forodha (Common External Tariff) na kuondosheana Vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru (Non-Tariff Barriers). Masuala hayo yamekuwa na mvutano kutokana na Nchi Wanachama kuweka maslahi ya kitaifa mbele zaidi kwani yanatishia uchumi wa nchi husika. Kadhalika, Waheshimiwa Mawaziri walitoa wito kwa Nchi Wanachama kuendeleza kuimarisha miundombinu ya barabara, reli, usafri wa anga na baharini, ili kurahisisha mzunguko huru wa

bidhaa na watu kwa kufikia utekelezaji wa kweli wa Itifaki ya Soko la Pamoja.

70. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kushiriki katika Mkutano wa Kamati ya kuondosheana Vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru (Non - Tariff Barriers - NTBs) ulifanyika tarehe 14 Febuari, 2020 Jijini Dar es Salaam, Tanzania. Katika Mkutano huo, Kamati ya NTBs ilijadili changamoto zinazowakabili wafanyabiashara na kupokea NTBs mpya na kuzitatua kwa ajili ya kuimarisha Biashara miongoni mwa Nchi Wananchama. Kadhalika, Mkutano wa Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ulifanyika Jijini Nairobi, Kenya tarehe 23 na 24 Septemba, 2019 na kufanya tathmini ya uhuru wa mzunguko wa bidhaa na huduma, watu na wafanyakazi, mitaji na haki ya Ukaazi na Kujiimarisha.

71. **Mheshimiwa Spika**, Mkutano wa Kilele wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (39$^{th}$ Ordinary Summit of SADC Heads of State and Government) umefanyika Jijini Dar es Salaam, Tanzania tarehe 17 na 18 Agosti, 2019. Mkutano huo, ulihudhuriwa na Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC kutoka nchi zote kumi na sita (16). Katika Mkutano huo Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alijumuika pamoja na Viongozi na Wakuu wa Nchi Wanachama.

72. **Mheshimiwa Spika,** Dhamira ya Mkutano huo ilikuwa ni "Kujenga Mazingira Wezeshi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na Jumuishi ya Viwanda, Kukuza Biashara na Ajira ndani ya Jumuiya ya SADC" (***A Conducive Environment of Inclussive and Sustainable Industrial Development, Increased Intra-Regional Trade and Job Creations).*** Sambamba na dhamira hiyo, Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC walijadili masuala mbali mbali ikiwemo kumchagua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja.

73. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Mkutano wa Kilele uliridhia Kiswahili kuwa lugha rasmi ya kazi ya SADC sambamba na Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kama tunavyoelewa lugha ya Kiswahili ilitumika katika ukombozi wa nchi za

Kusini mwa Afrika, hivyo lugha hiyo kupata umaarufu katika ukanda huo. SADC imeamua kuitunza heshima hiyo ya miaka mingi. Hivyo, wito kwa wananchi watumie vyema fursa hii ya lugha ya Kiswahili kupata ajira na fursa nyengine zinazotokana na Kiswahili. Vile vile, Mkutano wa Kilele ulihimiza nchi wanachama wa SADC wakamilishe mchakato wa kuondosheana Viza baina ya nchi zao.

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Mkutano huo ulitoa wito kwa Jumuiya ya Kimataifa kuiondoshea vikwazo vya kiuchumi nchi ya Zimbabwe ambavyo vinaathiri uchumi wa Nchi hio na upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wananchi. Kadhalika, Mkutano huo uliridhia kusainiwa kwa itifaki ya viwanda yenye lengo la kuimarisha maendeleo, uvumbuzi na ushindani wa viwanda katika ukanda wa nchi za SADC.

75. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa Pamoja wa Mawaziri wanaosimamia Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ulifanyika tarehe 25 Oktoba, 2019 Jijini Arusha, Tanzania. Masuala muhimu yaliojadiliwa ni pamoja na Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu (The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management and Sustainable Development) ya mwaka 2014 ambapo nchi tatu za Eswatini, Namibia na Afrika ya Kusini tayari zimeridhia itifaki hio.

76. **Mheshimiwa Spika,** mambo mengine yaliojadiliwa ni taarifa kuhusu Mkakati na Mpango Kazi wa SADC wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2015. Mkakati na Mpango Kazi huo unajumuisha masuala yaliyokubalika katika Mikataba ya Kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi, Mkataba wa Paris, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063.

77. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano ulipokea taarifa ya Mkakati wa Uchumi wa Bahari (SADC Blue Economy Strategy) ambao unajumuisha shughuli zinazotekelezwa katika bahari na maziwa ikiwa ni pamoja na uvuvi, mafuta na gesi, ufugaji wa samaki na utalii. Vile vile, mkutano huo ulijadili jitihada za kuimarisha mazingira, kulinda rasilimali na vivutio vya utalii, ili kuufanya

ukanda wa SADC kuvutia viumbe hai na binaadamu kuweza kuishi vizuri kwa kupunguza vihatarishi vya mazingira.

78. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo juu kuwa Zanzibar iliteuliwa kuwa ni miongoni mwa vituo vya kufanyia mikutano na matukio mbali mbali ya SADC katika kipindi hiki ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwenyekiti. Mkutano wa Kwanza wa Kukabiliana na Majanga ulifanyika Zanzibar tarehe 18 hadi 21 Februari, 2020 katika Hoteli ya Madinat Al Bahr Mkutano huo ulifunguliwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 21 Februari, 2019.

79. **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alitoa wito kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya SADC kuungana pamoja katika kukabiliana na maafa. Mkutano ulitathmini na kupendekeza mikakati na tahadhari za pamoja za kuzuia, kukabiliana na kupunguza ukubwa wa maafa yanayotokea katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya SADC. Mkutano huo umekubaliana kuwa na mashirikiano ya kupeana taarifa za tabianchi na hali ya hewa kwa kuanzisha kituo cha pamoja kitachokuwa kinatoa taarifa za awali **(Early Warning System Center).**

80. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa kumi na tisa wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya nchi zinazopakana na ukanda wa Bahari ya Hindi (The Indian Ocean Rim Association -IORA), ulifanyika Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu – UAE tarehe 5 hadi 7 Novemba 2019. Mkutano huo ulifanyika chini ya dhamira ***"Promoting a Shared Destiny and Path to Prosperity in the Indian Ocean".*** Mkutano huo uliiteua Umoja wa Falme za Kiarabu kuwa Mwenyekiti mpya wa Jumuiya hio kwa kipindi cha miaka miwili na Jamhuri ya Watu wa Bangladesh kuteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti.

81. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano huo uliridhia ombi la uwanachama la Jamhuri ya Maldives na kuifanya Jumuiya hio kuwa na jumla ya wanachama 22 **(Kiambatisho Nam. 5)**. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika Mkutano huo ni kuridhia vipaumbele vya Jumuiya kwa kipindi cha miaka miwili, ikiwa ni pamoja na kushirikiana katika kulinda usalama wa baharini, kurahisisha ufanyaji wa biashara na kuvutia uwekezaji, kuimarisha na

kubadilishana masuala ya kiutamaduni na utalii, kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuimarisha uchumi wa bahari.

82. **Mheshimiwa Spika,** Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wanatarajia kuanza utekelezaji wa Mkataba wa kuanzisha eneo huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) uliosainiwa mwaka 2018 Kigali, Rwanda ifikapo tarehe 1 Julai, 2020. Mkataba huo unajumuisha maeneo matano ya utekelezaji yakiwemo biashara ya bidhaa, biashara ya huduma, uwekezaji, haki miliki na Ushindani halali wa biashara. Katika Mkataba wa Soko Huru la Afrika zao la Karafuu limeingizwa katika kundi la bidhaa zitakazolindwa. Kulindwa kwa zao hilo, kutaiwezesha Zanzibar kuwa na soko la uhakika katika nchi za Afrika.

83. **Mheshimiwa Spika,** kuratibu na kushiriki katika Mikutano mbali mbali ya Kimataifa na Kikanda ya kisera, kisekta na kitaalamu; Zanzibar imeendelea kupata tija na kujenga uzoefu mkubwa. Kadhalika, Zanzibar inaendelea kutumia fursa ya soko la bidhaa zake pamoja na kuvitangaza vivutio vyake vya utalii katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa.

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa programu ya uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya nchi (Diaspora), Jukwaa la majadiliano na Wanadiaspora na Kongamano la sita la Wanadiaspora wa Tanzania lilifanyika tarehe 14 na 15 Disemba, 2019 katika Ukumbi wa Hoteli ya Verde iliyopo Unguja. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake ya ufunguzi alisisitiza kuhusu umuhimu wa kuwashirikisha Wanadiaspora katika maendeleo ya nchi yao ya asili na kuahidi kuwa Serikali itawasilisha katika Baraza la Wawakilishi Sheria ya Diaspora ya Zanzibar kabla ya mwezi Mei, 2020. Ninafuraha kuona kwamba Baraza la Wawakilishi limeshaipitisha Sheria hio katika kikao chake cha mwezi Aprili, 2020. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa namna mnavyoiunga mkono Serikali katika suala zima la Diaspora.

85. **Mheshimiwa Spika,** kupitia majadiliano na Wanadiaspora yanayofanyika kwa kutumia Makongamano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuwa na mashirikiano mema na Wanadiaspora na wameendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuwaletea mandeleo na kutoa huduma kwa wananchi. Kwa mfano; Ujumbe wa Madaktari kutoka Marekani ulifika

Zanzibar kutoa huduma za Afya kwa Wananchi kuanzia tarehe 5 hadi 9 Julai, 2019 katika Hospitali ya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba kupitia Jumuiya ya Wanadiaspora wa Tanzania wanaoishi Maryland - Marekani (Head Inc). Ujumbe huo ulijumuisha Madaktari, Wafamasia na Wauguzi. Madaktari hao wameendelea kuunga mkono jitahada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchangia maendeleo ya sekta muhimu ya afya ambapo wananchi wa Mkoa wa Kusini Pemba wamenufaika na huduma hizo.

86. **Mheshimiwa Spika,** katika kupambana na ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na Virusi vya CORONA Wanadiaspora wanaoishi Canada kupitia Jumuiya ya ZACADIA tarehe 23 Machi, 2020 wametoa msaada wa vitanda 12 kwa Wizara ya Afya, ili kusaidia wagonjwa wa COVID - 19 katika kituo cha kuhifadhia wagonjwa hao kilichopo Kidimni. Upatikanaji wa vifaa hivyo umewezesha kuongeza vifaa vya huduma vya kupambana na maradhi ya COVID - 19.

87. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano kati ya Wanadiaspora na Serikali umewezesha kuimarisha uhusiano na mashirkiano katika kukuza na kuendeleza uzalendo, kushajihisha maendeleo pamoja na kuthamini Nchi yao ya asili ikiwemo suala la kujitolea utaalamu wao. Tunatoa pongezi kwa Jumuiya zote za Wanadiaspora ambazo zinaendelea kuisaidia Zanzibar kwa njia moja au nyengine. Tunawaomba waendelee na moyo wao huo wa kuitunza na kuitukuza nchi yao ya asili.

**Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

88. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 2,771.8 kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS milioni 2,000.0 kwa Mradi wa Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 iliingiziwa TZS. milioni 1,954.3 sawa na asilimia 71 kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS milioni 995.0 sawa na asilimia 50 kwa Mradi wa Maendeleo.

89. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programu hii, wafanyakazi 18 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu, Uzamili, Stashahada ya Uzamili, Shahada, Stashahada na Astashahada

katika fani ya Sheria, Rasilimali Watu, Utawala wa Umma, Mawasiliano na Habari, Ushirikiano wa Kimataifa na Diplomasia, Utawala wa Biashara, Uhasibu na Uongozi na Utawala **(Kiambatisho Nam. 6)** kinatoa ufafanuzi. Aidha, wafanyakazi tisa (9) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya udereva wa Viongozi mashuhuri (VIP), Uhudumu na Ukarimu, Kompyuta, Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Sekta za Umma na Uhasibu.

90. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, mafunzo maalumu ya upishi na ukarimu yamefanyika yaliyowashirikisha wafanyakazi 45. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuanzia tarehe 11 Septemba hadi tarehe 10 Oktoba, 2019. Vile vile, wafanyakazi 100 wamepatiwa mafunzo juu ya athari za rushwa na uhujumu wa uchumi. Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalamu kutoka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA). Aidha, wafanyakazi sita (6) wamepatiwa mafunzo ya kujiandaa na kustaafu. Mafunzo hayo yamesaidia sana na wafanyakazi wamefahamu umuhimu wa kutekeleza wajibu wao wa kazi.

91. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha wafanyakazi kupima afya zao na namna ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza, mafunzo maalum yametolewa kwa wafanyakazi 100 ambayo yalikwenda sambamba na upimaji wa Sukari, Kifua Kikuu na Shindikizo la Damu. Mafunzo hayo yalitolewa na wataalamu kutoka Wizara ya Afya katika kitengo cha kisukari na maradhi yasiyoambukiza Zanzibar. Matokeo ya mafunzo hayo yanawafanya wafanyakazi kuwa imara kiafya kwa sababu ya kuangalia afya zao kila mwaka pamoja na kupata ushauri nasaha wa kujikinga na maradhi hayo.

92. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya vikao vitatu vya Kamati ya Uongozi na vikao vinne vya Kamati Tendaji vimeandaliwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa Sheria inavyoelekeza. Vikao hivyo vilijadili ripoti ya ufungaji wa hesabu za mwaka wa fedha 2018/2019, Mpango wa uingizwaji fedha, tathmini ya kikao cha utekelezaji wa mpango kazi, maandalizi ya Kongamano la Sita la Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi, Rasimu ya Sheria ya Diaspora na Sheria ya Mambo ya Rais. Kufanyika kwa vikao hivi kumewezesha kutekelezwa matakwa ya Kisheria ambayo

yanaelekeza kufanyika kwa vikao, ili kupata maamuzi ya pamoja katika kuendesha shughuli za Serikali.

93. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii Wafanyakazi 60 walipatiwa likizo na stahiki zao ikiwa ni haki yao ya Kisheria **(Kiambatisho Nam. 7)** kinatoa ufafanuzi. Vile vile, wafanyakazi wawili wamepatiwa mafao yao ya kustaafu baada ya kumaliza muda wao wa utumishi wa Umma. Nachukua nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi hao kwa kutumikia vyema muda wao wa utumishi na naamini wataendelea kutumikia Nchi yetu wakati wakiwa nje ya utumishi wa Umma.

94. **Mheshimiwa Spika,** Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mambo ya Rais Namba 5 ya 1993 na Kutunga Sheria mpya ya mambo ya Rais umewasilishwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi mwezi Aprili, 2020. Aidha, utafiti juu ya uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake umefanyika. Matokeo ya utafiti huo yataisaidia ORMBLM kupanga mikakati ya uelewa kwa wafanyakazi wake katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Shughuli nyengine zilizofanyika ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini wa kazi za kawaida na Mradi wa maendeleo. Ufuatiliaji huo ulipelekea utekelezaji mzuri wa shughuli zilizopangwa na changamoto zilizobainika zilipatiwa ufumbuzi.

95. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, tafiti ndogo za ndani zimefanyika zikiwemo; Utafiti wa kutathmini utekelezaji wa Mpango wa likizo kwa watumishi wa ORMBLM, Utafiti wa kutathmini utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Umma katika ORMBLM, Utafiti kuhusu tathmini ya changamoto za utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Mheshimiwa Rais na Utafiti kuhusu Makisio ya bei ya vitu viliyopangwa katika Mapango wa ORMBLM wa mwaka 2019/2020 kwa kuangalia matumizi halisi yaliyofanyika katika ununuzi wa vitu hivyo. Matokeo ya tafiti hizi yatasaidia kupanga mipango sahihi ya utekelezaji wa bajeti zijazo za ORMBLM.

96. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Jengo hilo linajengwa na wakandarasi kutoka Wakala wa Ujenzi. Nyumba tatu za maakazi ya Wasaidizi wa Mheshimiwa Rais moja Chake Chake na

mbili Micheweni zipo katika hatua za mwisho kukamilika chini ya mafundi kutoka Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Hatua za kudhibiti mmong’onyoko wa udongo katika Ikulu ya Mkoani zimefanikiwa kwa kujengwa ukuta wenye urefu wa mita 35. Kazi hio imefanywa na Wataalamu kutoka Kampuni ya Gibotel kutoka Arusha. Ujenzi wote huo umefanywa kupitia fedha zilizotengwa katika mradi wa maendeleo.

97. **Mheshimiwa Spika,** nyumba zote za Ikulu zilizopo Pemba zinaendelea kutoa huduma pamoja na kupatiwa vitendea kazi wa utekelezaji wa kazi za kila siku. Aidha, wafanyakazi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba wameendelea kupatiwa mafunzo, likizo na stahiki nyengine.

98. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Watumishi 3,722 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waliopo Unguja, Pemba na Tanzania Bara wamefanyiwa upekuzi. Kati ya hao 3,438 walifanyiwa upekuzi wa awali na 284 walifanyiwa upekuzi maalum **(Kiambatisho Nam. 8)** kinahusika. Vile vile, ukaguzi wa Kiusalama katika majengo ya Serikali na Taasisi nyeti umefanyika kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nam. 9**. Ushauri wa Kiusalama umetolewa katika maeneo yote yaliyokaguliwa. Kadhalika, semina juu ya Utunzaji wa Nyaraka na Udhibiti wa Siri za Serikali zilifanyika ambapo jumla ya Watumishi 647 kutoka katika Taasisi za Serikali wameshiriki kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nam. 10**. Matokeo ya kufanyika kwa semina hizo zimesaidia kuleta mabadiliko katika utunzaji wa Nyaraka za Serikali, utendaji wa Masjala katika Ofisi za Serikali na utunzaji wa majengo ya Ofisi za Serikali.

**Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu**

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii iliidhinishiwa TZS. milioni 592.4. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 iliingiziwa TZS. milioni 298.9 sawa na asilimia 50 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

100. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwa ni pamoja na kufanikisha vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu. Jumla ya vikao 49 vya Baraza la Mapinduzi vilifanyika na kuongozwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pamoja na mambo mengine, vikao hivyo vilijadili nyaraka mbali mbali zikiwemo za Sera tatu na Miswada ya Sheria 18 na kutolewa maamuzi. Miswada hiyo imewasilishwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi na baadae kuwa Sheria baada ya Mheshimiwa Rais kuitia saini. Sera zote zimeanza kutumika kama miongozo ya Serikali inavyoelekeza. **(Kiambatisho Nam. 11)** kinahusika.

101. **Mheshimiwa Spika,** wakati huo huo vikao 18 vimefanyika vya Kamati ya Baraza la Mapinduzi vya Katiba na Sheria, Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Kadhalika, vikao 36 vya Kamati ya Makatibu Wakuu vilifanyika kwa wakati ambavyo navyo vilijadili na kuzitolea maoni nyaraka zinazohusiana na Sera na Miswada ya Sheria na kuwasilishwa katika vikao vya Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi.

102. **Mheshimiwa Spika,** vikao 34 kati ya Mheshimiwa Rais na Viongozi wa ngazi za juu wa Wizara za SMZ vilifanyika. Vikao hivyo, pamoja na mambo mengine, vilijadili kwa kina utekelezaji wa Mpango kazi wa kila Wizara na kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa Umma katika kusimamia vyema dhamana na majukumu yao pamoja na kuona matumizi halisi ya fedha za Serikali.

103. **Mheshimiwa Spika,** jitihada za kuwajengea uwezo viongozi wa kisiasa na watendaji wa ngazi za juu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kufanyika kwa kupitia semina zilizotolewa kwa ajili yao. Kazi hio ya kuwajengea uwezo imefanywa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka katika Taasisi za hapa nchini na hata kutoka Jumuiya ya Kimataifa. Mafunzo

ya kujenga uwezo yalihusu katika maeneo ya Utawala Bora, shughuli za Zimamoto na Uokozi na kusimamia ipasavyo matumizi ya Ardhi na Rasilimali zisizorejesheka kwa Maendeleo Endelevu ya nchi yetu. Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa mwenyekiti katika semina hizo.

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti na Watendaji wa ngazi za juu walipata mafunzo juu ya masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation) na maarifa ya uongozi (Emotional Intelligence in Leadership). Mafunzo hayo, yaliendeshwa kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola (Common Wealth Secretariat).

**105. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika Programu hii, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein amemteua Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa Mwenyekiti wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini baada ya mwenyekiti wa awali kupangiwa majukumu mengine.

**106. Mheshimiwa Spika,** kazi za ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji mipango kazi ya Wizara 15 umefanyika sambamba na kufanyika kwa tathmini maalum ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa Zanzibar. Ripoti ya tathmini hizo tayari imeshawasilishwa kwa Mamlaka inayohusika kwa ajili kufanyiwa kazi zaidi. Matarajio yetu ni kuwa utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo na Maamuzi yanayotolewa na Serikali utaendelea kuimarika na kuwa wenye ufanisi. Kiujumla, napenda kutoa wito kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali kuendelea kutoa ushirikiano stahiki kwa kitengo hiki, ili lengo la kuanzishwa kwake liweze kufikiwa.

**Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi**

**107. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 1,539.7. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Programu hii iliingiziwa TZS. milioni 1,131.1 sawa na asilimia 73 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**108. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii, umepelekea Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kupata mafanikio makubwa yakiwemo kuimarika kwa mazingira ya kazi pamoja na uwezo wa watumishi. Uwezo huo umeimarika kutokana na Ofisi kuendeleza programu za kuwajengea uwezo wa kitaalamu watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Jumla ya wafanyakazi watano (5) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na Shahada ya kwanza za fani ya Sera na Utafiti, Uongozi na Utawala pamoja na Manunuzi na Ugavi. Vile vile, wafanyakazi tisa (9) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Itifaki na Ukarimu, Ukatibu Mukhtasi, Uhasibu na Ukaguzi pamoja na mafunzo ya maisha baada ya kustaafu. Sambamba na hilo, wafanyakazi wengine 45 wamepatiwa taaluma ya namna ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza na maradhi ya VVU/UKIMWI.

## 3. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**109. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 itaendelea kutekeleza Programu Kuu 5 na Programu Ndogo 11.

**110. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Fungu A01 na A02 imetengewa jumla ya TZS. milioni 11,801.1 zikijumuisha mishahara, matumizi ya kazi za kawaida na mradi wa maendeleo. Fungu A01 limetengewa jumla ya TZS. milioni 9,563.5. Kati ya hizo TZS. milioni 8,063.5 kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS. milioni 1,500.0 kwa mradi wa maendeleo. Fungu A02 limetengewa jumla ya TZS. milioni 2,237.6 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

**111. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuratibu shughuli na kusimamia huduma za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

ii. Kuratibu na kusimamia mikutano kati ya Mheshimiwa Rais na viongozi wa Wizara za SMZ, ili kujadili utekelezaji wa Mipango ya kazi ya Wizara,
iii. Kuratibu na kusimamia majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake,
iv. Kuimarisha mawasiliano ya Ikulu,
v. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na maamuzi ya Serikali,
vi. Kushirikiana na Diaspora katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii,
vii. Kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi,
viii. Kuwawezesha wananchi kupata taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali yao,
ix. Kuwawezesha watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushiriki katika mtangamano wa Jumuiya za Kikanda yenye kuleta tija kwa Zanzibar,
x. Kuwawezesha watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufanya tafiti mbali mbali,
xi. Kuendeleza ujenzi wa nyumba za Serikali na matengenezo ya nyumba za makaazi ya Mheshimikwa Rais,
xii. Kuimarisha mazingira na usalama katika nyumba za Ikulu zilizopo Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma,
xiii. Kuimarisha usalama kwa watumishi wa Serikali na maeneo wanayofanyia kazi na
xiv. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

## 4. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**112. Mheshimiwa Spika,** Programu, vipaumbele na shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zitatekelezwa na Ofisi na Idara zifuatazo:-

i. Ofisi ya Faragha ya Rais (inahusika na Huduma za Mheshimiwa Rais; Ofisi ya Rais Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais),
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi,
iii. Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu,
iv. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi,
v. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
vi. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
vii. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba na
viii. Ofisi ya Usalama wa Serikali.

**113. Mheshimiwa Spika,** Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A01 ni kama zifuatazo:-

***1. Programu ya Kuratibu Shughuli na Kusimamia Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu***

**114. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuratibu shughuli, kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais na kuimarisha mawasiliano yatakayowawezesha wananchi kuendelea kupata taarifa za shughuli za kimaendeleo zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wake. Matokeo ya Programu hii ni kuendeleza Taswira nzuri ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli na kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais na
ii. Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi.

**115. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais,
ii. Kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais,

iii. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala katika Ofisi za Washauri wa Mheshimiwa Rais,
iv. Kutoa huduma za uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Faragha ya Rais,
v. Kutoa huduma za Uendeshaji kwa Viongozi Wastaafu,
vi. Kuimarisha Maktaba ya Mheshimiwa Rais,
vii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi,
viii. Kusimamia huduma katika nyumba za makaazi ya Mheshimiwa Rais katika Ikulu zilizopo Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma,
ix. Kukuza mawasiliano baina Wananchi na Wahusika wengine wa habari kupitia televisheni na redio,
x. Kutayarisha, kuchapisha na kusambaza majarida na machapisho maalum ya Ikulu na
xi. Kuimarisha mawasiliano kupitia mitandao ya kijamii na kutathmini matumizi ya TEHAMA katika ORMBLM.

**116. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Kuratibu Shughuli na Kusimamia Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 4,222.8 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

### *2. Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi*

**117. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha, kuendeleza ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi katika maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya nchi yao ya asili. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuendelea kufaidika kwa Zanzibar na fursa za Kiuchumi na Kijamii zinazotokana na Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa na

ii. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.

**118. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kushiriki katika Mikutano ya Kikanda ndani ya nchi,
ii. Kushiriki katika Mikutano ya Kikanda nje ya nchi,
iii. Kusimamia shughuli za kila siku za Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi,
iv. Kujenga uelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na Jumuiya za mtangamano wa Kikanda (EAC, SADC, IORA, AfCFTA na AU),
v. Kujenga Ushirikiano wa Kimataifa,
vi. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu,
vii. Kujenga uelewa kwa jamii juu ya Sera na Sheria ya Diaspora Zanzibar na utekelezaji wake,
viii. Kuandaa Jukwaa la Wanadiaspora na
ix. Kushiriki katika mikutano ya ndani na kimataifa inayohusiana na Diaspora.

***3.*** **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 743.3 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

### *3. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*

**119. Mheshimiwa Spika,** malengo makuu ya Programu hii ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Kuimarisha Shughuli za Mipango, Kuandaa na Kuchambua Sera na Kufanya tafiti; Kuimarisha Usalama wa Serikali na

Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika zaidi kwa mazingira ya utendaji kazi pamoja na ufuatiliaji wa shughuli za ORMBLM. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo nne zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM,
ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM,
iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM – Pemba na
iv. Programu Ndogo ya Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma.

**120. Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa sambamba na mradi wa ujenzi na matengenezo ya nyumba za Ikulu.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuandaa na kuratibu mikutano ya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
ii. Kutoa huduma za Uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi,
iv. Kuendesha vikao vya Bodi ya Zabuni vya ORMBLM,
v. Kufanya Ukaguzi wa hesabu za awali na endelevu na Vikao vya Kamati ya Ukaguzi,
vi. Kuandaa Mkutano wa kutunuku Nishani,
vii. Kufanya utafiti juu ya ushiriki na tija kwa Zanzibar katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa,
viii. Kufanya utafiti juu ya mtazamo wa Jamii kuhusu Wanadiaspora,
ix. Kufanya utafiti juu ya njia zitakazotumika katika kuzalisha na kuhifadhi takwimu na matumizi yake,
x. Kufanya utafiti juu ya Athari za Mmong'onyoko wa Ardhi katika Nyumba za Ikulu pamoja na Gharama za kudhibiti,
xi. Kufanya matengenezo ya jengo la Ikulu ya Mnazi mmoja,

xii. Kujenga nyumba ya Nyumba za wafanyakazi Viongozi Mashuhuri (VIP) katika Ikulu ya Dodoma,
xiii. Kuimarisha huduma katika Ikulu za Chake Chake, Mkoani na Micheweni,
xiv. Kutoa huduma za Uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba,
xv. Kufanya Upekuzi wa Kiusalama wa awali na endelevu kwa wafanyakazi,
xvi. Kufanya Ukaguzi wa Kiusalama wa Majengo na Miundombinu ya Serikali na
xvii. Kuandaa Mafunzo na warsha juu ya utunzaji wa Siri na Udhibiti wa Nyaraka kwa watumishi wa Serikali.

**122. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 3,097.4 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii na TZS. milioni 1,500.0 kwa ajili ya mradi wa maendeleo.

**123. Mheshimiwa Spika,** Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A02 ni hizi zifuatazo:-

### *4. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu*

**124. Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuimarika Sera, Sheria na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, Maendeleo na kuimarisha uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma. Vile vile, kuhakikisha malengo na majukumu ya Wizara na Taasisi za Serikali yanatekelezwa ipasavyo na kufikiwa kwa ufanisi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na kudumisha amani na umoja Nchini. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

i. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Baraza la Mapinduzi na Majukumu ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi/Katibu Mkuu Kiongozi na

ii. Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma.

**125. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kutayarisha vikao vya kawaida vya BLM na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Makatibu Wakuu,
ii. Kutayarisha vikao Maalum vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake,
iii. Kusimamia Programu za mafunzo ya kujenga uwezo kwa Viongozi wa Kisiasa na Kiutendaji watakaoteuliwa mara baada ya Uchaguzi Mkuu,
iv. Kuwapatia nyenzo na miongozo ya kufanyia kazi Viongozi na Watendaji Wakuu watakaoteuliwa mara baada ya Uchaguzi Mkuu,
v. Kutayarisha mikutano kati ya Mheshimiwa Rais na Wizara za SMZ kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa Mipangokazi,
vi. Kuimarisha Uhusiano na Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya na majukwaa ya Kikanda na Kimataifa,
vii. Kujenga uwezo kwa watumishi wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini na
viii. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya BLM na Kamati zake pamoja na masuala maalum yanayohusu Sera, Sheria na Maamuzi ya Serikali.

***126.*** **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 805.5 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

### *5. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi*

**127. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni Kuimarisha Mazingira ya Kazi, kuongeza Ujuzi na ufanisi wa Wafanyakazi. Matokeo ya utekelezaji

wa Programu hii ni kuwa na mfumo bora na wa kisasa wa kuendesha shughuli za Ofisi ya Baraza la Mapinduzi na Uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo moja ifuatayo:-

i. Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

**128. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

i. Kuimarisha miundombinu ya Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, majengo pamoja na mazingira yake,

ii. Kuimarisha huduma za mawasiliano na utekelezaji wa kazi za kila siku za Ofisi ya Baraza la Mapinduzi,

iii. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Sekretarieti na wafanyakazi wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi,

iv. Kutoa taaluma ya afya na namna bora ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza pamoja na VVU/UKIMWI,

v. Kuimarisha huduma za Kitengo cha Uandaaji, Usambazaji na Uhifadhi wa Kumbukumbu za BLM na

vi. Kuongeza ari na bidii za wafanyakazi kwa kulipa mishahara na stahiki zao.

**129. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 1,432.1 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

## 5. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**130. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi

ya Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zenye jumla ya TZS. milioni 11,801.1. Kati ya fedha hizo, TZS. milioni 10,301.1 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. milioni 1,500.0 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika **Kiambatisho Nam. 12.**

131. **Mheshimiwa Spika,** matarajio ya upatikanaji wa fedha hizi kwa ORMBLM itapelekea kutimiza majukumu yake katika maeneo yafuatayo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa maagizo na ahadi za Mheshimiwa Rais,
ii. Kuiwezesha Serikali kutimiza wajibu wake wa Kikatiba na Kisheria kwa ajili kupanga mipango, kutunga sera na sheria za kuleta maendeleo kwa wananchi,
iii. Kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Serikali,
iv. Wananchi kupata taarifa mbali mbali za utekelezaji wa shughuli za Serikali na kukuza taswira ya Mheshimiwa Rais,
v. Kuimarika kwa Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na Ushiriki wa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi katika shughuli za maendeleo na
vi. Ustawi wa huduma kwa wananchi wetu na kuratibu usimamizi wa amani na utulivu, ili kuendeleza umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi.

## 6. HITIMISHO

132. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena naomba kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa umahiri katika kuingoza nchi yetu vyema katika vipindi vyote vya uongozi wake. Umahiri na umakini alionao Mheshimiwa Rais wetu umechangia kwa kiasi kikubwa katika kudumisha Amani na Utulivu nchini mwetu. Vile vile, naomba nimpongeze tena Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa juhudi mbali mbali alizozifanya katika kuhakiksha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 inatekelezwa kikamilifu. Sote ni mashahidi kuwa mambo mengi yaliyoainishwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020 tayari yameshatekelezwa.

**133. Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kuwa nchi yetu inategemea kufanya Uchaguzi Mkuu mwishoni mwa mwaka huu. Naomba kusisitiza suala la umuhimu wa kufuata sheria za nchi na kudumisha Amani na Utulivu wakati wa kuelekea katika harakati za Uchaguzi Mkuu. Napenda kuwakumbusha kuwa hakuna mbadala wa Amani maana ikitoweka ni gharama kubwa kuirudisha. Amani na Utulivu ni tunu na hazina kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe na Wananchi wote kwa ujumla kuithamini Amani na Utulivu tuliyonao na tuulinde kwa gharama yeyote ile.

**134. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi chote cha miaka kumi ya awamu ya saba, ORMBLM imewatumikia wananchi kwa uadilifu mkubwa. Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametuongoza katika kuwatumikia wananchi kuondosha kero zao na kuhakikisha maendeleo yanapatikana kwa haraka. ORMBLM inawahakikishia wananchi kwamba fikra za kimaendeleo zilizoasisiwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume, Serikali inaziendeleza inazienzi, inazilinda na kutekelezwa kwa vitendo. Malengo ya ORMBLM ni kuhakikisha kuwa Nchi inakuwa imara na yenye kujitegemea kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**135. Mheshimiwa Spika,** pongezi zangu za dhati nazipeleka kwa wananchi wa Jimbo letu la Chwaka ambao wamenichagua kuwa Mwakilishi wao kwa ustahamilivu wao kwangu wakati natekeleza majukumu ya Kitaifa ya Uwaziri. Katika kipindi chote hicho hawakusita kushirikiana nami katika kuandaa utaratibu mzuri wa kutekeleza ahadi nilizowaahidi. Vile vile, tulishirikiana ipasavyo katika kuibua na kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbali mbali zilizolikabili Jimbo letu. Napenda kulithibitishia Baraza lako Tukufu kuwa kutokana na ushirikiano wetu tumepata ufanisi mkubwa katika kupiga hatua za maendeleo katika Jimbo letu.

**136. Mheshimiwa Spika,** hii ni bajeti yetu ya mwisho katika Serikali ya Awamu ya saba kabla ya kuingia kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka huu. Kutokana na hilo, nachukua fursa hii kukushukuruni kwa dhati kabisa kwa namna mlivyoisimamia Serikali katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 na mlivyojitolea

kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kupitia majimbo yenu. Nakupongezeni nyote kwa kutimiza ahadi mlizozitoa katika Majimbo yenu wakati mkiomba ridhaa ya kuchaguliwa na wananchi. Naomba niwatakie kila la kheri kwa wale wote wenye nia ya kugombea katika Uchaguzi ujao. Aidha, kwa wale ambao wameamua kustaafu nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajaalie maisha mema na furaha na tuwe pamoja katika kuijenga nchi yetu.

137. **Mheshimiwa Spika,** miaka mitano ni mingi kukaa na binadamu mwenzako. Hivyo, kwa niaba yangu binafsi na kwa Ofisi yetu kama kuna Mheshimiwa au Mjumbe yeyote ambae tumemkwaza katika kutekeleza majukumu yetu ya ORMBLM, tunamuomba atusamehe kwani haikuwa dhamira yetu bali ni kasoro katika kutekeleza wajibu wetu; kwa upande wenu, hakuna mlichotukosea. Nawaomba tuendelee kufanya kazi tukiwa wamoja kwa maslahi ya wananchi wetu.

138. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima, nawashukuru Viongozi pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kipindi chote nilichoongoza na kusimamia kazi hizi walinipa ushirikiano wao wa dhati ambao uliniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Salum Maulid Salum, Katibu Mkuu ORMBLM, Ndugu Haroub Shaib Mussa, Katibu wa Rais, Ndugu Salmin Amour Abdallah, Naibu Katibu Baraza la Mapinduzi, Ndugu Salum Kassim Ali, Naibu Katibu Mkuu ORMBLM, Ndugu Maryam Haji Mrisho, Naibu Katibu wa Rais, Dkt. Juma Yakout Juma, Naibu Katibu Msaidizi Baraza la Mapinduzi, Wakurugenzi, Wasaidizi wa Rais na Watumishi wengine.

139. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa naomba pia kuwashukuru Washauri wa Mheshimiwa Rais ambao ni Mheshimiwa Abdulrahman Mwinyi Jumbe, Mheshimiwa Burhan Saadat Haji, Mheshimiwa Zainab Omar Mohammed, Mheshimiwa Chimbeni Kheir Chimbeni, Mheshimiwa Dk. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Abdalla Rashid Abdalla na Mheshimiwa Ali Mzee Ali. Nakuombeni Viongozi wezangu na Wafanyakazi wengine tuendelee kufanya kazi kwa bidii na weledi, ili tulinde mafanikio tuliyoyapata na tufikie matarajio ya wananchi kwa Ofisi yetu. Naomba tuendelee kuifanyia kazi kwa vitendo kauli ya Mheshimiwa Rais isemayo **"tusifanye kazi kwa mazoea"**.

**140. Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote wa kuwasilisha hotuba hii. Ni matumaini yangu kuwa mtatoa ushauri na michango mizuri itakayosaidia utekelezaji wa majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

**141. Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza kusoma hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi naomba kuchukua fursa hii kukushukuruni kwa namna ambavyo tumeshirikiana katika kufanikisha majukumu yetu. Tuombeane kheri, baraka na fanaka katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani (Ramadhan Kareem). Namuomba Mwenyezi Mungu, Subhanahu Wa Taala, atuondoshee mitihani ya maradhi na atuzidishie neema katika Nchi yetu.

**142. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu liipokee, liijadili na kutushauri na hatimae liipitishe Bajeti hii.

**143. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**(Issa Haji Ussi Gavu)**
Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
Zanzibar.

**Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida 2019/2020**

| JINA LA IDARA | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2019/2020 | FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ZA MIEZI TISA 2019/2020 | ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA | ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi ya Faragha ya Rais | Kusimamia Huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais | 3,723,814,000 | 2,831,241,689 | 2,608,164,066 | 70 | 92 |
| Idara ya Mawasiliano - Ikulu | Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi | 450,498,000 | 366,224,006 | 328,710,567 | 73 | 90 |
| | **Jumla** | **4,174,312,000** | **3,197,465,695** | **2,936,874,633** | **70** | **92** |
| Ofisi ya Baraza la Mapinduzi | Programu Ndogo 1: Uratibu wa Shughuli za BLM na Majukumu ya KBLM/KMK | 477,855,000 | 366,384,625 | 221,827,530 | 46 | 61 |
| | Programu Ndogo 2: | 114,538,000 | 92,010,750 | 77,050,750 | 67 | 84 |

| JINA LA IDARA | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2019/2020 | FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ZA MIEZI TISA 2019/2020 | ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA | ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma | | | | | |
| | **Jumla** | **592,393,000** | **458,395,375** | **298,878,280** | **50** | **65** |
| | Programu Ndogo: Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza La Mapinduzi | 1,539,707,000 | 1,187,024,875 | 1,131,071,540 | 73 | 95 |
| | **Jumla** | **2,132,100,000** | **1,645,420,250** | **1,429,949,820** | **67** | **87** |
| Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari | Kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kikanda na Kimataifa | 415,003,000 | 313,937,803 | 263,485,791 | 63 | 84 |

| JINA LA IDARA | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2019/2020 | FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ZA MIEZI TISA 2019/2020 | ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA | ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanaoishi Nje | Kuratibu shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi | 233,320,000 | 194,623,734 | 202,306,315 | 87 | 104 |
| | **Jumla** | **648,323,000** | **508,561,537** | **465,792,106** | **72** | **92** |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi | 1,426,269,000 | 1,136,481,790 | 954,881,055 | 67 | 84 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM | 2,348,650,000 | 1,227,998,990 | 1,213,401,877 | 52 | 99 |

| JINA LA IDARA | PROGRAMU NDOGO | BAJETI KWA MWAKA WA 2019/2020 | FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA | FEDHA ZA MIEZI TISA 2019/2020 | ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA | ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba | Kuratibu na kusimamia shughuli za ORMBLM – Pemba | 806,335,000 | 617,547,840 | 675,554,290 | 84 | 109 |
| Ofisi ya Usalama wa Serikali (G.S.O) | Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma | 190,510,000 | 139,840,000 | 105,507,331 | 55 | 75 |
| | **Jumla** | **4,771,764,000** | **3,121,868,620** | **2,949,344,553** | **62** | **94** |
| | **Jumla** | **11,726,499,000** | **8,473,316,102** | **7,781,961,112** | **66** | **92** |

**Kiambatisho Nam. 2: Wageni Waliofika Ikulu Kuonana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia Mwezi Julai 2019 hadi Mwezi Aprili, 2020**

| TAREHE | JINA LA MGENI | CHEO |
|---|---|---|
| **AGOSTI, 2019** | | |
| 09.08.2019 | Bwana Tirso Dos Santos | Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu ya Sayansi na Utamaduni (UNESCO) nchini Tanzania |
| 13.08.2019 | Kamishna Mohamed Haji Hassan | Kamishna wa Polisi - Zanzibar |
| 18.08.2019 | Mheshimiwa Ramadhan Dau | Balozi wa Tanzania nchini Indonesia |
| 20.08.2019 | Bibi Jacqueline Mahon | Mwakilishi Mkaazi wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa Unaoshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) nchini Tanzania |
| | Bwana Alvaro Rodriguez | Mwakilishi Mkaazi wa Mpango wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Miradi ya Maendeleo (UNDP) nchini Tanzania |
| 22.08.2019 | Lt. Jenerali Yakoub H. Mohamed | Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) |
| 27.08.2019 | Mheshimiwa Eugine Kayihura | Balozi wa Jamhuri ya Rwanda nchini Tanzania |
| 30.08.2019 | Commodore Hassan Mussa Mzee | Mkuu wa Kikosi cha KMKM |
| **SEPTEMBA, 2019** | | |
| 08.09.2019 | Mhe. Marcelino Medina Gonzalez | Naibu Waziri wa Kwanza wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Cuba na Ujumbe wake |
| 09.09.2019 | Bwana Nishant Dighe | Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya RAK GAS |

| | | |
|---|---|---|
| 10.09.2019 | Bwana Dong Weihong | Katibu wa Kamati ya Chama Cha Kikomunisti cha China na Makamo Mkuu wa Taasisi ya "China National Research Institute of Food and Fermentation Industries Co. Ltd" akifuatana na Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China aliyepo Zanzibar |
| 16.09.2019 | Dkt. Zakia Mohamed Abubakar | Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) |
| 16.09.2019 | Dkt. Abdulla Juma Abdulla | Naibu Katibu Mkuu wa CCM - Zanzibar |
| 17.09.2019 | Mheshimiwa Rini M. Soemarno | Waziri anayeshughulikia Mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Indonesia pamoja na Ujumbe wake |
| 19.09.2019 | Mheshimiwa Azali Assoumani | Rais wa Comoro |
| **OKTOBA, 2019** | | |
| 07.10.2020 | Maj. General (Mst.) S.S. Omar | Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini |
| 17.10.2019 | Mheshimiwa Omar Othman Makungu | Jaji Mkuu wa Zanzibar |
| 24.10.2019 | Mheshimiwa Hamid Mahmoud | Jaji Mkuu Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi |
| 25.10.2019 | Mheshimiwa Guo Yezhou | Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China pamoja na Ujumbe wake |
| **NOVEMBA, 2019** | | |
| 01.11.2019 | Dkt. Charles Massambu | Rais wa Chama cha Wapathologia Tanzania (APT) akufuatana na :<br>- Prof. Said Aboud : Makamo wa Rais<br>- Dk. Mtebe Majigo : Katibu |

| | | |
|---|---|---|
| | | - Prof. James Kitinya : Mjumbe na Mshauri<br>- Dk. Edward Kabyemela : Mjumbe<br>- Prof. Eligius Lyamuya : Mjumbe<br>- Dr. Emael Moshi : Mjumbe<br>- Prof. Amos Mwakigonja : Mjumbe |
| 04.11.2019 | Mheshimiwa CHO Taeick | Balozi wa Jamhuri ya Korea nchini Tanzania |
| 07.11.2019 | Mheshimiwa Jaji Sylvain Ore | Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (African Court on Human and Peoples' Rights) akifuatana na Ujumbe wake kutoka nchini Kenya, Tunisia,<br>Mozambique, Cameroun, Rwanda, Malawi, Algeria, Republic of Congo, Nigeria, Burkina Faso na Tanzania |
| 17.11.2019 | Bwana Mustapha Berraf | Rais wa Umoja wa Kamati za Olympiki za Afrika (Association of National Olympic Committees of Africa) na Ujumbe wake |
| 22.11.2019 | Bwana Evindn Hansen | Afisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland nchini Norway akifuatana na :<br>- Dk. Randi-Luise Mogster : Naibu Afisa Mtendaji Mkuu<br>- Dk. Dohn Wigum Dahil : Mkurugenzi wa Idara ya Uhusiano wa Kimataifa<br>- Dk. Trond Mohn : "Philanthropist"<br>- Bibi Marit Mohn Westlake : Mtaalamu<br>- Bibi Mona Schramn : Mtaalamu<br>- Bibi Louise Mohan : Mtaalamu<br>- Bwana Ole P. Maaloy : Mtaalamu |

| | | |
|---|---|---|
| | | - Bwana Robert Westlake : Mtaalamu<br>- Bwana Hans Joachim Schramn : Mtaalamu pamoja na Viongozi wa Wizara ya Afya - Zanzibar |
| 25.11.2019 | Bibi Christine Musisi | Mwakilishi Mkaazi wa Mpango wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Miradi ya Maendeleo (UNDP) nchini Tanzania |
| 26.11.2019 | Dkt. Bashiru Ali Kakurwa | Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi |
| **DISEMBA, 2019** | | |
| 03.12.2019 | Sheikh Saleh Omar Kabi | Mufti wa Zanzibar |
| 04.12.2019 | Bwana Pham Minh Chinh | Mjumbe na Katibu wa Kamati Kuu ya Uongozi wa Chama cha Kikomunisti cha Vietnam |
| **FEBRUARI, 2020** | | |
| 06.02.2020 | Mheshimiwa Sandro Agostinho de OLIVEIRA | Balozi wa Angola nchini Tanzania |
| 13.02.2020 | Bwana Abdulmajid Mussa Nsekela | Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB akifuatana na :<br>- Dk. Ally Laay : Mwenyekiti wa Bodi<br>- Bwana Mbwana Ahmed : Meneja wa Benki ya CRDB, Tawi la Zanzibar<br>- Bibi Tully Esther Mwambapa : Mkurugenzi Masoko wa Benki ya CRDB |
| 14.02.2020 | Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) | Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayeshughulikia Muungano na Mazingira |
| 21.02.2020 | Dkt. Stergomena L. Tax | Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini |

| | | |
|---|---|---|
| | | mwa Africa (Southern Africa Development Community – SADC) |
| **MACHI, 2020** | | |
| 02.03.2020 | Prof. Florens D. Luoga | Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (B.O.T) na Ujumbe wake |
| 03.03.2020 | Mheshimiwa Xie Xiaowu | Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China aliyepo Zanzibar |
| 05.03.2020 | Mheshimiwa Dk. Sahabu Isa Gada | Balozi wa Nigeria nchini Tanzania akifuatana na Ujumbe wa Wafanyabiashara kutoka Nigeria:<br>- Mhe. Yabo Faruk Malami<br>- Bibi Bintu Bwala Ekikor<br>- Bwana Ibru Emmanuel<br>- Bwana Ibru Peter Akpovbovbo<br>- Bwana Ovbagbedia Innocent Adams<br>- Bwana Boer Dutse James<br>- Bwana Oladimeji Michael Olusegun |
| 10.03.2020 | Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb) | Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| | Bibi Nasra M. Hilal | Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwanaharakati Bibi Siti Bint Saad pamoja na Ujumbe wake |
| 16.03.2020 | Mheshimiwa Bhagwant Singh | Balozi Mdogo wa India aliyepo Zanzibar |
| 23.03.2020 | Mheshimiwa Panya Ali Abdalla | Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa akifuatana na:<br>- Mheshimiwa Ali Suleiman Shihata: Makamu Mwenyekiti |

| | | |
|---|---|---|
| | | - Mheshimiwa Mtumwa Suleiman Makame: Mjumbe<br>- Mheshimiwa Rashid Ali Juma: Mjumbe<br>- Mheshimiwa Ame Haji Ali: Mjumbe<br>- Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu: Mjumbe<br>- Mheshimiwa Viwe Khamis Abdalla: Mjumbe<br>- Bibi Karima Abdul Wahab: Katibu<br>- Bwana Talib Enzi Talib: Katibu |

**Kiambatisho Nam. 3: Orodha ya vipindi vilivyorushwa hewani na Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu – Zanzibar kupitia Kituo cha ZBC Radio (A)**

| NAM | JINA LA KIPINDI | TAREHE YA KURUSHWA HEWANI |
|---|---|---|
| 1 | Utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Pemba - Wanadiaspora Pemba | 7/3/2019 |
| 2 | Maoni ya wananchi ujenzi wa barabara ya Ukongoroni na Charewe | 7/9/2019 |
| 3 | Maendeleo ya ujenzi wa majengo mapya ya ofisi za Serikali - Gombani | 7/17/2019 |
| 4 | Maonesho ya Kilimo Kizimbani JKU | 8/12/2019 |
| 5 | Elimu ya Utumiaji wa Rasilimali ya Mchanga – JKU | 8/26/2019 |
| 6 | Ziara ya Dk ukaguzi wa vifaa vya kutengenezea barabara Kibele | 9/9/2019 |
| 7 | Maendeleo ya Ujenzi wa barabara Kibonde Mzungu | 9/28/2019 |
| 8 | Uimarishaji wa Huduma za Wazee | 10/7/2010 |
| 9 | Maendeleo ya Ujenzi wa Skuli 9 za SMZ | 10/14/2019 |
| 10 | Maendeleo ya Kijijiji cha Mgonjoni | 10/21/2019 |
| 11 | Maendeleo ya ujenzi wa barabara za Ole - Kengeja, Wawi - Mabaoni na Mkanyageni - Kangagani | 10/28/2019 |
| 12 | Uzinduzi wa Meli ya Mafuta ya Ukombozi II | 12/2/2019 |
| 13 | Mapinduzi II kutimia miaka mitano | 12/9/2019 |
| 14 | Maendeleo ya Ujenzi wa barabara za Pemba | 12/16/2019 |
| 15 | Kongamano la Sita la Diaspora Tanzania 2019 | 12/25/2019 |
| 16 | Uzinduzi wa Skuli 9 za Sekondari | 1/29/2020 |
| 17 | Ufunguzi wa Mradi wa Maji Safi na Mazingira - Saateni | 2/12/2020 |
| 18 | Ufunguzi wa Daraja la Dk Ali Mohamed Shein - Kibonde Mzungu | 2/19/2020 |

| NAM | JINA LA KIPINDI | TAREHE YA KURUSHWA HEWANI |
|---|---|---|
| 19 | Ufunguzi wa ujenzi wa barabara ya Bububu – Mkokotoni | 3/4/2020 |
| 20 | Maendeleo ya ujenzi wa vyuo vya amali vya Kibuteni na Makunduchi | Uhariri unaendelea |

**Vipindi Vilivyorushwa na Radio Jamii**

| NAM | MAUDHUI YA KIPINDI | REDIO HUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | Afya Corona | Mtegani FM |
| 2 | Udhalilishaji | Mtegani FM |
| 3 | Muamko wa jamii - Elimu | Redio Tumbatu |
| 4 | Maedeleo ya Uvuvi | Redio Tumbatu |

**Vipindi vya Televisheni ZBC (B)**

| NAM | JINA LA KIPINDI | TAREHE YA KURUSHWA HEWANI |
|---|---|---|
| 1 | Utoaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Pemba - Wanadiaspora Pemba | 7/4/2019 |
| 2 | Maoni ya wananchi ujenzi wa barabara ya Ukongoroni na Charewe | 7/10/2019 |
| 3 | Maendeleo ya ujenzi wa majengo mapya ya ofisi za Serikali - Gombani | 7/18/2019 |
| 4 | Maonesho ya Kilimo Kizimbani JKU | 8/13/2019 |
| 5 | Elimu ya Utumiaji wa Rasilimali ya Mchanga – JKU | 8/27/2019 |
| 6 | Ziara ya Dk ukaguzi wa vifaa vya kutengenezea barabara Kibele | 9/10/2019 |
| 7 | Maendeleo ya Ujenzi wa barabara Kibonde Mzungu | 9/29/2019 |
| 8 | Uimarishaji wa Huduma za Wazee | 10/8/2010 |

| NAM | JINA LA KIPINDI | TAREHE YA KURUSHWA HEWANI |
|---|---|---|
| 9 | Maendeleo ya Ujenzi wa Skuli 9 za SMZ | 10/15/2019 |
| 10 | Maendeleo ya Kijijiji cha Mgonjoni | 10/22/2019 |
| 11 | Maendeleo ya ujenzi wa barabara za Ole - Kengeja, Wawi - Mabaoni na Mkanyageni - Kangagani | 10/29/2019 |
| 12 | Uzinduzi wa Meli ya Mafuta ya Ukombozi II | 12/3/2019 |
| 13 | Mapinduzi II kutimia miaka mitano | 12/10/2019 |
| 14 | Maendeleo ya Ujenzi wa barabara za Pemba | 12/17/2019 |
| 15 | Kongamano la Sita la Diaspora Tanzania 2019 | 12/26/2019 |
| 16 | Tamasha la siku ya mazoezi kitaifa | 1/2/2020 |
| 17 | Ziara za Mapinduzi za Dk Shein (Kipindi Maalumu) | 1/11/2020 |
| 18 | Mradi wa umwagiliaji Kinyasini | 1/16/2020 |
| 19 | Uzinduzi wa Skuli 9 za Sekondari | 1/30/2019 |
| 20 | Ufunguzi wa Mradi wa Maji Safi na Mazingira - Saateni | 2/13/2020 |
| 21 | Ufunguzi wa Daraja la Dk Ali Mohamed Shein - Kibonde Mzungu | 2/20/2020 |
| 22 | Ufunguzi wa Mkutano wa Mawaziri SADC | 2/21/2020 |
| 23 | Ufunguzi wa ujenzi wa barabara ya Bububu - Mkokotoni | 3/5/2020 |
| 24 | Uwekaji wa jiwe la Msingi Skuli ya Sekondari ya Wingwi | 3/12/2020 |
| 25 | Jukwaa la 10 la biashara | 3/7/2020 |
| 26 | Dk Shein na wasanii | 3/12/2020 |

| NAM | JINA LA KIPINDI | TAREHE YA KURUSHWA HEWANI |
|---|---|---|
| 27 | Ziara ya Dk Shein Binguni | 3/26/2020 |
| 28 | Maendeleo ya ujenzi wa vyuo vya amali vya Kibuteni na Makunduchi | Uhariri unaendelea |

**Kiambatisho Nam. 4: Orodha ya Shehia zilizooneshwa Sinema**

| NAM | KIJIJI KILICHOONESHWA SINEMA | SHEHIA | TAREHE YA KUONESHWA SINEMA |
|---|---|---|---|
| 1 | Mbaleni | Kitope | 9/6/2019 |
| 2 | Donge Karange | Donge | 9/7/2019 |
| 3 | Kiembeni | Dunga | 9/8/2019 |
| 4 | Hanyegwa Mchana | Jendele | 9/9/2019 |
| 5 | Mtende | Mtende | 9/10/2019 |
| 6 | Kizimkazi | Dimbani | 9/11/2019 |
| 7 | Kiboje | Ghana | 9/12/2019 |
| 8 | Chimba | Chimba | 9/13/2019 |
| 9 | Kiuyu Mbuyuni | Kiuyu | 9/14/2019 |
| 10 | Pembeni | Pembeni | 9/15/2019 |
| 11 | Ndagoni | Ndagoni | 9/16/2019 |
| 12 | Mgelema | Ndagoni | 9/17/2019 |
| 13 | Kendwa | Nanguji | 9/18/2019 |
| 14 | Chambani | Chambani | 9/19/2019 |
| 15 | Mgonjoni | Kilombero | 12/2/2019 |
| 16 | Kinduni | Kinduni | 12/3/2019 |
| 17 | Kichungwani | Kitope | 12/4/2019 |

| NAM | KIJIJI KILICHOONESHWA SINEMA | SHEHIA | TAREHE YA KUONESHWA SINEMA |
|---|---|---|---|
| 18 | Kitope | Kitope | 12/6/2019 |
| 19 | Kilombero | Kilombero | 12/7/2019 |
| 20 | Pale | Pale | 12/8/2019 |
| 21 | Njia ya Mtoni | Donge | 12/10/2019 |
| 22 | Pangatupu | Bumbwini | 12/11/2019 |
| 23 | Makoba | Bumbwini | 12/12/2019 |
| 24 | Mbiji | Donge | 12/13/2019 |
| 25 | Mikarafuuni | Kinyasini | 2/20/2020 |
| 26 | Maziwani | Maziwani | 2/21/2020 |
| 27 | Mtambwe | Bwagamoyo | 12/22/2020 |
| 28 | Ukutini | Ukutini | 2/23/2020 |
| 29 | Mvumoni | Mvumoni | 2/24/2020 |

**Kiambatisho Nam. 5: Majina ya nchi wanachama za Jumuiya ya IORA**

1. Iran,
2. Australia,
3. Bangladesh,
4. Comoro,
5. India,
6. Indonesia,
7. Kenya,
8. Madagascar,
9. Malaysia,
10. Mauritius,
11. Msumbiji,
12. Oman,
13. Ushelisheli,
14. Singapore,
15. Somalia,
16. Afrika Kusini,
17. Sri Lanka,
18. Tanzania,
19. Thailand,
20. Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE),
21. Yemen na
22. Jamhuri ya Maldives

**Kiambatisho Nam. 6: Idadi ya Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo**

**Mafunzo ya Muda Mrefu**

| **NAM.** | **IDARA/ OFISI** | **ASTASHAHADA** | | **STASHAHADA** | | **STASHAHADA YA JUU** | | **SHAHADA YA KWANZA** | | **STASHAHADA YA UZAMILI** | | **SHAHADA YA PILI** | | **SHAHADA YA UZAMIVU** | | **JUMLA** | **FANI** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | | |
| 1 | OFISI YA FARAGHA NA HUDUMA ZA RAIS | | | | | | | | | | | | | | **1** | **1** | Sheria za Kimataifa |
| 2 | BARAZA LA MAPINDUZI | | | | | | | 1 | 1 | 1 | | 2 | | | | **5** | Manunuzi na Ugavi,mawasiliano na Habari, Mipango, Uongozi, Maendeleo ya Sera, Uchumi |

| NAM. | IDARA/ OFISI | ASTASHAHADA | | STASHAHADA | | STASHAHADA YA JUU | | SHAHADA YA KWANZA | | STASHAHADA YA UZAMILI | | SHAHADA YA PILI | | SHAHADA YA UZAMIVU | | JUMLA | FANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | | |
| 3 | IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI | | | | | | | | | | | | | | | **0** | |
| 4 | IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI | | | | | | | | 1 | | | 2 | | | | **3** | Uongozi wa Rasilimali Watu, Sheria na Utawala wa Umma. |
| 5 | IDARA YA MAWASILIANO - IKULU | | | | | | | | | | | | 1 | | | **1** | mawasiliano na Habari |
| 6 | IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA | | 1 | | | | | | | | | 1 | 1 | | | **3** | Ushirikiano wa Kimataifa na Diplomasi |

| NAM. | IDARA/ OFISI | ASTASHAHADA | | STASHAHADA | | STASHAHADA YA JUU | | SHAHADA YA KWANZA | | STASHAHADA YA UZAMILI | | SHAHADA YA PILI | | SHAHADA YA UZAMIVU | | JUMLA | FANI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | **Me** | **Mke** | | |
| | WAZANZIBARI WALIOKO NJE | | | | | | | | | | | | | | | | a |
| 7 | OFISI YA AFISA MDHAMINI ORMBLM - PEMBA | | | | | | | 1 | 1 | | | | | | | **2** | Uongozi wa Rasilimali Watu, Utawala wa Biashara (Uhasibu) |
| **JUMLA** | | **0** | **1** | **0** | **0** | **0** | **0** | **2** | **3** | **1** | **0** | **5** | **2** | **0** | **1** | **15** | |

**Mafunzo ya Muda Mfupi na mafunzo ya ndani ya kazi**

| NAM. | IDARA | ME | MKE | JUMLA | FANI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | OFISI YA FARAGHA YA MHESHIMIWA RAIS | 1 | | 1 | Udereva |
| | | 2 | 5 | 7 | Kujiandaa na kustahafu |
| | | 20 | 20 | 40 | Rushwa na uhujumu wa uchumi |
| | | 20 | 20 | 40 | Maradhi yasioambukiza |
| | | 5 | 8 | 13 | Uandaaji vyakula |
| 2. | BARAZA LA MAPINDUZI | 2 | 2 | 4 | Uandaaji vyakula |
| | | 2 | 0 | 2 | Udereva |
| | | 6 | 4 | 10 | Protocol |
| | | 1 | 2 | 3 | Kujiandaa na kustahafu |
| | | 3 | 4 | 7 | Rushwa na uhujumu wa uchumi |
| | | 3 | 4 | 7 | Maradhi yasioambukiza |
| 3. | IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI | 2 | 1 | 3 | Rushwa na uhujumu wa uchumi |
| | | 3 | 1 | 4 | Maradhi yasioambukiza |
| 4. | IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI | 1 | | 1 | Udereva |
| | | 4 | 2 | 6 | Kujiandaa na kustahafu |
| | | 16 | 20 | 36 | Rushwa na uhujumu wa uchumi |
| | | 1 | 0 | 1 | Uhasibu na fedha |
| | | 16 | 20 | 36 | Maradhi yasioambukiza |
| 5. | IDARA YA MAWASILIANO - IKULU | 1 | 0 | 1 | Kujiandaa na kustahafu |
| | | 4 | 3 | 7 | Maradhi yasioambukiza |
| 6. | IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA WAZANZIBARI WALIOKO NJE | 5 | 2 | 7 | Kujiandaa na kustahafu |
| | | 3 | 4 | 7 | Maradhi yasioambukiza |
| 7. | OFISI YA AFISA MDHAMINI ORMBLM - PEMBA | 3 | 3 | 6 | Kompyuta na Uhudumu na ukarimu. |
| | **JUMLA** | **124** | **125** | **249** | |
| | **JUMLA KUU** | | | **264** | |

**Kiambatisho Nam. 7: Idadi ya Watumishi waliokwenda likizo**

| NAM. | JINA LA OFISI NA IDARA | ME | MKE | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Faragha ya Mheshimwa Rais | 18 | 16 | 34 |
| 2. | Ofisi ya Baraza la Mapinduzi | 17 | 10 | 27 |
| 3. | Idara ya Mawasiliano na Habari –Ikulu | 1 | 1 | 2 |
| 4. | Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi | 2 | 0 | 2 |
| 5. | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 2 | 6 | 8 |
| 6. | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 0 | 0 | 0 |
| 7. | Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba | 5 | 3 | 8 |
| | **JUMLA KUU** | **45** | **36** | **81** |

**Kiambatisho Nam. 8: Idadi ya wafanyakazi waliofanyiwa Upekuzi na Taasisi walizotoka**

**Upekuzi wa Awali**

| NAM. | WIZARA/TAASISI | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | BARAZA LA WAWAKILSHI | 12 |
| 2. | BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ) | 37 |
| 3. | BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB) | 40 |
| 4. | CHUO CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA) | 01 |
| 5. | CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA) | 14 |
| 6. | KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA | 10 |
| 7. | KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO) | 3 |
| 8. | MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI | 08 |
| 9. | MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA) | 39 |
| 10. | MAMLAKA YA MANUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA | 12 |
| 11. | MAMLAKA YA MKONGA WA TAIFA | 1 |
| 12. | MAMLAKA YA UDHIBITI WA MAJI NA NISHATI (ZURA) | 15 |
| 13. | MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) | 18 |
| 14. | MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE | 8 |
| 15. | MAMLKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE | 9 |
| 16. | MFUKO WA BARABARA | 3 |
| 17. | OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR | 64 |
| 18. | OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA | 10 |
| 19. | OFISI YA MKUU WA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA | 33 |
| 20. | OFISI YA MKUU WA MKOA WA KUSINI UNGUJA | 37 |
| 21. | OFISI YA MKUU WA MKOA WA KJINI MAGHARIBI | 13 |
| 22. | OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI | 12 |
| 23. | OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI | 44 |

| NAM. | WIZARA/TAASISI | IDADI |
|---|---|---|
| 24. | OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI | 23 |
| 25. | OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ | 548 |
| 26. | SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) | 08 |
| 27. | SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR (ZIC) | 05 |
| 28. | SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA | 20 |
| 29. | SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI | 9 |
| 30. | SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR | 27 |
| 31. | SHIRIKA LA NYUMBA | 3 |
| 32. | SHIRIKA LA UMEME (ZECO) | 23 |
| 33. | SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) | 58 |
| 34. | SKULI YA JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) | 18 |
| 35. | TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA | 03 |
| 36. | TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) | 03 |
| 37. | TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR (ZEC) | 94 |
| 38. | WAHANDISI WA FANI MBALI MBALI | 50 |
| 39. | WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI | 22 |
| 40. | WIZARA YA AFYA | 510 |
| 41. | WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI | 46 |
| 42. | WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA | 17 |
| 43. | WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI | 1,038 |
| 44. | WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO | 44 |
| 45. | WIZARA YA HABARI, UTALII NA MAMBO YA KALE | 67 |
| 46. | WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO | 71 |
| 47. | WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI | 179 |
| 48. | WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO | 109 |
| | **JUMLA** | **3,438** |

**Upekuzi Maalum**

| NAM. | WIZARA/TAASISI | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA) | 18 |
| 2. | KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA (ZPDC) | 9 |
| 3. | MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) | 16 |
| 4. | OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR | 27 |
| 5. | OFISI YA MTAKWIMU MKUU | 2 |
| 6. | SHIRIKA LA BANDARI | 94 |
| 7. | SHIRIKA LA MELI | 21 |
| 8. | SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) | 14 |
| 9. | SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR | 27 |
| 10. | SHIRIKA LA UTANGAZAJI (ZBC) | 10 |
| 11. | TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA | 10 |
| 12. | TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR (ZEC) | 25 |
| 13. | WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII | 08 |
| 14. | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA | 03 |
| 15. | **JUMLA** | **284** |

## Kiambatisho Nam. 9: Orodha ya Taasisi Zilizofanyiwa Ukaguzi wa Kiusalama

1. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi – Pemba,
2. Makaazi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi – Pemba,
3. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja,
4. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A,
5. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B,
6. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Karume Haouse,
7. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Dar es Salaam,
8. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) – Pemba na
9. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pamja na Ofisi za Wilaya za Wete na Micheweni.

**Kiambatisho Nam. 10: Idadi Watumishi Waliopewa Mafunzo ya Udhibiti wa Siri na Utunzaji wa Nyaraka za Serikali**

| NAM. | WIZARA/TAASISI | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB) | 52 |
| 2. | MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA | 58 |
| 3. | OFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI PEMBA | 25 |
| 4. | OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA (DPP) | 08 |
| 5. | OFISI YA MKUU WA MKOA WA KASKAZINI PEMBA PAMOJA NA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA WETE NA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA MICHEWENI. | 34 |
| 6. | SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) UNGUJA, PEMBA NA DAR ES SALAAM | 174 |
| 7. | TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR | 22 |
| 8. | TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR (ZEC) | 63 |
| 9. | WAKALA WA UCHAPAJI WA SERIKALI (Semina maalum kwa washiriki wa zoezi la mitihani ya Taifa) | 80 |
| 10. | WIZARA YA AFYA | 131 |
| | **JUMLA** | **647** |

## Kiambatisho Nam. 11: Orodha ya Nyaraka za Sera na Sheria zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi

| NAM | SERA/SHERIA |
|---|---|
| 1. | Sera ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu |
| 2. | Sera ya kuendeleza zao la nazi Zanzibar |
| 3. | Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali Zanzibar |
| 4. | Sheria ya Sekta binafsi ya ulinzi ya mwaka 2019 ( The private Sector Security Servises Act, 2019) |
| 5. | Sheria ya Kulinda taarifa binafsi, 2019 ( The Personal Data Protection Act,2019) |
| 6. | Mswada wa Sheria ya kuanzishwa wakala wa Serikali mtandao Zanzibar |
| 7. | Mswada wa marekebisho ya Sheria ya Mufti Nambari 9 mwaka 2019 |
| 8. | Mswada wa Sheria ya kuanzishwa wakala wa Ujenzi na Utunzaji wa barabara |
| 9. | Mswada wa marekebisho ya Sheria na Usafiri Barabarani kwa madhumuni ya kuanzisha Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani |
| 10. | Rasimu ya Mswada wa Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa vitendo (Law School of Zanzibar) |
| 11. | Rasimu ya Sheria ya Mswada wa wazee Zanzibar |
| 12. | Mapendekezo ya kufanyiwa Mapitio kwa Sheria ya Mizani na Vipimo Nambari 4 ya mwaka 1983 |
| 13. | Mapendekezo ya kutungwa Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa mifugo Zanzibar |
| 14. | Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar nambari 8 ya mwaka 2012 na kutunga Sheria Mpya ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar |
| 15. | Rasimu ya Sheria ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar |
| 16. | Mapendekezo ya kutunga Sheria Mpya ya Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, 2020. |
| 17. | Mswada wa Sheria ya Mambo ya Rais |
| 18. | Sheria ya Diaspora |
| 19. | Mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Wataalamu wa Maabara ya Afya na Mambo Mengine yanayohusiana na Nayo |

| | |
|---|---|
| 20. | Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mizani na Vipimo na Kuanzishwa Wakala wa kushughulikia Masuala ya Mizani na Vipimo |
| 21. | Mswada wa kufuta Sheria ya Vileo ya mwaka 1920 na kuanzishwa Sheria ya Udhibiti, Usimamizi, Usafirishaji, Uhifadhi, Uuzaji, Usambazaji na Utumiaji wa Vileo na Mambo yenye kuhusiana na hayo ya mwaka 2020. |

## Kiambatisho Nam. 12: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti 2020/2021

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | UENDESHAJI OFISI (OC) | MATUMIZI YA MAENDELEO | MAPENDEKEZO 2020/2021 |
|---|---|---|---|---|
| **Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu** | **2,336,609,088** | **1,886,185,700** | **0** | **4,222,794,788** |
| Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli na kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais | 2,187,814,088 | 1,569,113,700 | 0 | 3,756,927,788 |
| Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi | 148,795,000 | 317,072,000 | 0 | 465,867,000 |
| **Usimamizi wa Majukumu ya Kikanda na Kisheria ya Baraza la** | **0** | **805,479,645** | **0** | **805,479,645** |

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | UENDESHAJI OFISI (OC) | MATUMIZI YA MAENDELEO | MAPENDEKEZO 2020/2021 |
|---|---|---|---|---|
| **Mapinduzi** | | | | |
| Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na majukumu ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi | 0 | 676,027,500 | - | 676,027,500 |
| Ufuatiliaji na Tathmini ya utendaji kazi wa Taasisi za Umma | 0 | 129,452,145 | - | 129,452,145 |
| **Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi** | **976,900,000** | **455,220,355** | **0** | **1,432,120,355** |
| Utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi | 976,900,000 | 455,220,355 | 0 | 1,432,120,355 |
| **Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi** | **139,528,002** | **603,794,768** | **0** | **743,322,770** |
| Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na | 139,528,002 | 330,474,768 | 0 | 470,002,770 |

| PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO | MSHAHARA | UENDESHAJI OFISI (OC) | MATUMIZI YA MAENDELEO | MAPENDEKEZO 2020/2021 |
|---|---|---|---|---|
| Kimataifa | | | | |
| Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi | | 273,320,000 | 0 | 273,320,000 |
| **Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** | **1,352,162,910** | **1,745,219,532** | **1,500,000,000** | **4,597,382,442** |
| Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi | 703,420,800 | 867,459,298 | 0 | 1,570,880,098 |
| Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM | 83,895,360 | 274,755,000 | 1,500,000,000 | 1,858,650,360 |
| Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM - Pemba | 564,846,750 | 402,407,000 | 0 | 967,253,750 |
| Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma | | 200,598,234 | 0 | 200,598,234 |
| **JUMLA KUBWA** | **4,805,200,000** | **5,495,900,000** | **1,500,000,000** | **11,801,100,000** |